**MWINYI:** Risasi 728 zilitumika mauaji kiwanda cha sukari

UKURASA 5



**MABOMU** ya machozi yapigwa wananchi wakitelekeza jeneza

UKURASA 4


Uteuzi wa Queen Sendiga RC Iringa...

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

MILTON OBOTE Rais aliyeacha historia ya kupinduliwa, akarejea Ikulu

UCHAMBUZI

RAZA atoa ya moyoni

- Ataka maridhiano, majadiliano
- Tume ya Fedha za Muungano

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Mei 19, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0580585

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# NYUNDO ZA SAMIA POLISI

## **AAGIZA** matibabu kwanza PF3 baadaye, ujambazi kutumbua ma-RPC, kibano madereva wazembe...

*Endelea Ukurasa 2*

# IGP SIRRO AMWONDOA KAMANDA MAMBOSASA DAR ES SALAAM

UKURASA 3



SACP Camilius Wambura    SACP Lazaro Mambosasa



Rais Samia Suluhu Hassan akikagua kazi za upimaji na ukataji wa vitambaa vinavyotumika kushona sare za Jeshi la Polisi, baada ya kuzindua kiwanda cha ushonaji nguo cha jeshi hilo, Kurasini, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 5

## MKURANGA WATAHADHARISHWA KUONEKANA SIMBA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Alberto Sanga, ametoa wito kwa wakazi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari kutokana na taarifa za kuonekana kwa simba wawili...

UKURASA WA 7

## WANAFUNZI WANAOCHOMA MAJENGO SHULE KUKIONA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, amelitaka Jeshi la Zimamoto na ...

## KIKWETE ATAJA DAWA UHABA WA WATUMISHI

UKURASA 3

**MICHEZO** MASHABIKI WAIPOKEA GEITA GOLD FC KIFALME UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK. 6

# ... aahidi kutatua kero Jeshi la Polisi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali itashughulikia vikwazo vya kiutendaji vinavyolikabili Jeshi la Polisi.

Miongoni mwa vikwazo hivyo vilivyowasilishwa kwake na Mkuu wa Jeshi hilo (IGP), Simon Sirro, ni uhaba wa askari na miundombinu mizuri ya makazi ya askari wao.

Rais Samia alitoa ahadi hiyo jana alipofungua kiwanda cha ushonaji sare za Jeshi la Polisi mkoani Dar es Salaam.

"Hii ikiwa ni kumbukumbu kwetu sote, kwani aliyeweka jiwe la msingi hapa ni Hayati Dk. John Magufuli, na ni mradi ambao ulikuwa wa mwisho kwake kabla ya kifo chake. Hii inaonyesha tunavyoendelea kumuenzi," alisema Rais Samia.

Alisema serikali inaunga mkono juhudi za Jeshi la Polisi katika kujiimarisha, ikiwamo kuanzisha kiwanda hicho ambacho kinatarajia kushona sare za jeshi hilo zipatazo 125,200 na kuagiza vikosi vyote vya jeshi kukikutumia kiwanda hicho kutengeneza sare zao pamoja na kampuni binafsi na taasisi nyingine.

"Mradi huu ambao umejengwa kwa fedha ambazo Jeshi la Polisi wanasema ni za 'task force' na kutekelezwa na jeshi lenyewe, imefanya gharama halisi iwe Sh. milioni 666.4 badala ya Sh. bilioni 1.4 ambazo zingetumika iwapo angepewa mkandarasi.

"Nimefurahi kwamba sasa ushonaji huu utafanywa nanyi Jeshi la Polisi badala ya mtu kutoka nje ya nchi. Pia muwape Jeshi la Magereza wawatengenezee viatu na vikosi vingine vije kushona sare kwenu.

"Kila fursa iliyopo kwa kikosi kingine itumiwe ipasavyo kuinua uchumi wa kikosi kingine," aliagiza Rais Samia.

Aliwataka kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kusimamia nidhamu na kulinda taswira ya Jeshi la Polisi nchini.

"Serikali itaendelea kuongeza vituo vya polisi pamoja na makazi, itahakikisha inazingatia hilo, jeshi liongeze kasi ya kukuza uchumi ili kuondoa kero," alisema Rais Samia.

Awali IGP Sirro alisema mradi huo ulizinduliwa Mei 30, mwaka jana na kiwanda hicho kitachukua watendaji 50 kikiwa na vyerehani 200.

Sirro akizungumzi kuhusu hali ya usalama nchini, alisema kwa ujumla kuna utulivu ingawa kuna matukio kadhaa ambayo yanaendelea kudhibitiwa kama ujambazi, ukatili wa kijinsia na udhalilishaji.

"Uhalifu umepunguzwa kwa asilimia 13 na ajali zimepungua kwa asilimia 29.1. Hali ya nidhamu ipo imara isipokuwa wapo baadhi wanaokiuka na wanadhibitiwa," alisema Sirro.

Alibainisha kuwa kutokana na jeshi hilo na kuwa na takribani askari 43,000, wanatarajia kuanzisha kiwanda cha maji Desemba mwaka huu.

IGP Sirro alimshukuru Rais kwa kufanikisha jeshi hilo kuwalipa wastaafu wa jeshi hilo kiasi cha Sh. bilioni 6.4, fedha ambazo walikuwa hawajalipwa kwa muda mrefu.

Alimwomba Rais kutoa kibali cha ajira za askari polisi wapya ili kukabiliana na uhaba wa watumishi uliopo, ukichagizwa na kustaafu na kufariki dunia kwa watumishi.

# Ujambazi kutumbua ma-RPC

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema udhibiti wa ujambazi utakuwa miongoni mwa vigezo vitakavyotumika katika kuteua na kutengua nafasi za makamanda wa polisi wa mikoa (ma-RPC).

Amesema baada ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kukutana na makamanda wa Polisi Mei 8, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, anatarajia juhudi kuongezwa katika kukabiliana na uhalifu huo.

"Kuna ambao wanataka kurejesha ujambazi, wanapima kina cha maji, zipo taarifa ya hawa watu wanaanza kubonyeza, ninaomba pawe pagumu, hawa watu wasiweze kubonyeza, muwe imara kukabiliana na wanaotaka kuwajaribu. Hapo awali mliweza kukabiliana nao, sasa hivi kwa nini msiweze?" Alihoji.

Rais alikuwa kwenye uzinduzi wa kiwanda cha kushona sare za Jeshi la Polisi kilichoko Kurasini mkoani Dar es Salaam jana.

Alisema miongoni mwa vigezo atakavyovitumia kabla ya kufanya uteuzi au kutengua nafasi za makamanda wa polisi wa mikoa ni udhibiti wa ujambazi kwenye maeneo yao.

"Vigezo vitakavyotumia katika kuteua na kutengua makamanda wa mikao ni hali ya udhibiti wa ujambazi... ninajua IGP umeniletea majina kadhaa," alisema.

Kuhusu matukio yanayoendelea kushamiri nchini ukiwamo udhalilishaji wa kijinsia, Rais alisema kuna ongezeko kutokana na takwimu za jeshi hilo kuonyesha Januari hadi Aprili mwaka jana, matukio yalikuwa 398 na mwaka huu ni 458 kwa kipindi kama hicho.

"Nitoe wito kwa jamii kutoa usimamizi wa malezi, sababu yanatokea kwenye maeneo yetu, mambo yanafichwa, wanaotenda matukio hayo watakuwa wanaona hawachukuliwi sheria na wataendelea," aliagiza.

Rais alilitaka jeshi hilo kuzifuta kesi ambazo zimekaa muda mrefu na kukosa ushahidi wa kuzipeleka mahakamani ili kupunguza mrundikano wa mahabusu nchini.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifuta kesi 147, Jeshi la Polisi mnaweza kufanya hivyo.

"Jana (juzi) nilipoapisha majaji, niligusia uharaka wa kesi na uchunguzi uharakishwe. Polisi ipunguze kesi za kibambikiza kutokana na wengine kesi kukosa ushahidi, polisi pia mfute kesi hizo.

"Mahabusu wengi wapo kesi haziendi, wanasubiriwa kuhukumiwa, jeshi jikagueni kupunguza idadi ya mahabusu gerezani," aliagiza.

Awali, IGP Sirro alisema jeshi hilo linatilia mkazo katika uadilifu miongoni mwa watendaji wake na wanaokiuka huchukuliwa hatua za kinidhamu.



Mwendesha pikipiki maarufu bodaboda, akiwa amewapakia wanafunzi watano katika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kitendo ambacho ni hatari na uvunjaji wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais aagiza matibabu kwanza, PF3 baadaye

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kutazamwa kwa sheria inayotaka watu wanaopata ajali na kuumizwa katika matukio ya uhalifu kuwa na taarifa ya polisi (PF3) ili kutibiwa, kwa kuwa ina dosari.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana alipofungua kiwanda cha ushonaji sare za Jeshi la Polisi kilichoko Kurasini mkoani Dar es Salaam.

"Wanaopata ajali wanaumia katika viwango tofauti wengine wanahitaji huduma ya haraka. Hahudumiwi bila PF3, sheria ndiyo ipo lakini iangaliwe mtu apate huduma ndipo atafute PF3, wanaomwokota baada ya ajali hawakumbuki kuanzia polisi, bali hospitali, tunawapoteza watu sababu ya vipengele hivi," aliagiza.

Rais pia aliliagiza Jeshi la Polisi kuanzisha mfumo maalum wa kielektroniki utakaowabaini madereva wanaofanya makosa kila mara barabarani ili kuwafutia leseni zao.

Pia, aliliagiza jeshi hilo kutoa elimu zaidi kwa umma kuhusu usalama barabarani, ili zifahamike badala ya sheria hizo kuwa mtego wa ukusanyaji mapato.

Aliagiza mfumo wa kielektroniki uanzishwe kuwezesha kila kosa linalofanywa na madereva kuonekana nchi nzima na kuingizwa katika orodha ya makosa yanayojirudia ili kutoa fursa ya adhabu sahihi kwa madereva hao.

"Kosa likifanywa na dereva mmoja lionekane nchi nzima, kwamba akifanya makosa manne ndipo afutiwe leseni. Kuliko ilivyo sasa anafanya makosa mikoa tofauti tofauti na rekodi hakuna na yanajirudia.

**WIZI MTANDAONI**

Rais alibainisha kutoridhishwa na hatua zinazochukuliwa dhidi ya wezi wa mtandaoni, akihoji kulikuwa na ulazima gani kusajili laini za simu kwa kutumia vidole kama bado kuna utapeli na wizi mtandaoni.

"Mbona hatuoni wanaofanya makosa hayo? Mbona hawafikishwi mahakamani wanaofanya uhalifu huo, wanatumia mtandao gani? Jeshi mshirikiane na TCRA na taasisi za kifedha, kampuni za simu kushughulikia wizi wa mtandoni," aliagiza.

Alihimiza ushirikiano wa kipolisi kikanda na kimataifa ili kushughulikia uhalifu wa dawa za kulevya, biashara haramu ya binadamu na ugaidi.

HABARI KITAIFA

# JK ataja mwarobaini uhaba wa walimu nchini

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, ameshauri serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kuunganisha shule zote kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuhakikisha zote zinaunganishwa na mtandao wa intaneti.

Alitoa ushauri huo jana wakati akifungua mkutano wa kimataifa wa kujadili namna ya kuboresha sekta ya elimu uliohudhuriwa na wadau kutoka nchi mbalimbali.

Alisema endapo shule zote nchini zitaunganishwa na intaneti, itakuwa imemaliza pia tatizo la upungufu wa walimu lililopo hasa katika eneo la sayansi.

"Dunia inabadilika, sasa hivi kila kitu kinaunganishwa na kufanyika kupitia TEHAMA, kwa hiyo hata mfumo wetu wa elimu tunatakiwa tuupeleke kibunifu zaidi, tunahitaji kutumia teknolojia hii, kila shule iunganishwe na intaneti na hili linawezekana," alisema Kikwete.

Alisema kuna haja ya kujifunza pia kwa nchi nyingine mbinu zinazotumika katika kuboresha mifumo yao ya elimu.

"Kwa mfano mwaka jana baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona, wakati vyuo na shule zetu zikufungwa huku kwetu, baadhi ya nchi masomo yaliendelea na wanafunzi walihitimu kama kawaida online kwa sababu walitumia TEHAMA," alisema.

"Wakati wanafunzi wetu vyuoni wakishangilia baada ya serikali kutangaza kufungwa na wanafunzi kwenye shule zetu za msingi na sekondari wakicheza rede mtaani baada ya shule kufungwa, wenzetu waliendelea kama kawaida kwa njia ya mtandao. Hiki ndicho tunapaswa kufanya na huku kwetu."

"Dunia inabadilika na huko tuendako kila kitu kitakuwa kinafanyika kwa njia ya kidijitali, tunachotakiwa kufanya na sisi ni kuhakikisha tunaweka ubunifu zaidi katika kutumia teknolojia hii ya TEHAMA kwenye mfumo wetu wa elimu, tusitegemee tu kwamba lazima tuwe na bajeti kubwa ya fedha katika kufanikisha hili, kinachotakiwa ni kuweka ubunifu zaidi na inawezekana."

Kikwete alisema uwekezaji katika elimu unatakiwa ufanywe kwa kushirikiana na wadau wote na si kuiachia serikali peke yake.

"Ndio maana nyie wadau wa elimu mpo, hakikisheni mnajifunza na kwa nchi nyingine namna wao wanavyofanya katika kuboresha mfumo wao wa elimu kuwa wa kidijitali zaidi na mshirikiane na serikali kuboresha na huku kwetu," alisema Kikwete.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), John Kalaghe, alisema ni vema uwajibikaji wa kila mtu katika sekta hiyo ya elimu italeta matokeo mazuri.




Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akifungua mkutano wa kimataifa wa elimu bora ulioandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TenMeT), mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sirro amwondoa Mambosasa Dar

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amefanya mabadiliko katika uongozi wa jeshi hilo, ikiwamo kumhamisha aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Lazaro Mambosasa kwenda makao makuu Dodoma.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi Camillius Wambura anachukua nafasi ya Kamanda Mambosasa ya Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

Msemaji wa jeshi hilo, David Misime, akizungumza na Nipashe jana, alisema IGP Sirro alifanya mabadiliko hayo juzi.

Alisema Kamanda Mambosasa anakwenda Makao Makuu ya Upelelezi, Dodoma kuwa Mkuu wa Kitengo cha Operesheni.

Misime alibainisha kuwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, amehamishwa kwenda kuwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda Maalum Dar es Salaam, kuchukua nafasi ya Kamishna wa Polisi Salum Hamdun ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Kamishna wa Msaidizi wa Polisi, Longinus Tibishibwamu, amekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara.


BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB)

MIKUTANO YA MASHAURIANO NA WADAU WA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA 2021

"Juhudi za Makusudi za Wadau Kuwezesha Ukuaji wa Makandarasi wa ndani".

Dar es Salaam; Tarehe 27 - 28 Mei 2021, Ukumbi wa Diamond Jubilee
Mwanza; Tarehe 10 - 11 Juni 2021, Ukumbi wa Gold Crest

Bodi ya Usajili wa Makandarasi (**CRB**) inapenda kuwataarifu **Makandarasi** na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wakiwemo **Waajiri, Wataalam Washauri** (Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi) na wataalam mbalimbali katika sekta ya ujenzi kuwa imeandaa mikutano ya kikanda ya mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi katika mikoa ya **Dar es Salaam (Tarehe 27 - 28 Mei 2021 Ukumbi wa Diamond Jubilee)** na **Mwanza (Tarehe 10 - 11 Juni 2021, Ukumbi wa Gold Crest),** Katika vituo vyote, mikutano itaanza saa 2.00 asubuhi. Kaulimbiu ya mikutano ni: **"Juhudi za Makusudi za Wadau Kuwezesha Ukuaji wa Makandarasi wa ndani"**.; na mada zifuatazo zitajadiliwa:-

- Uzoefu wa CRB kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi nchini
- Mtazamo wa Makandarasi kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wao
- Tathmini ya Utekelezaji wa vifungu wezeshi vya sheria ya manunuzi ya umma kwa ukuaji wa makandarasi
- Mtazamo wa Waajiri kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi
- Uzoefu wa wataalam washauri kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi
- Uzoefu wa Makandarasi wa kigeni kuhusu changamoto zinazowakabili makandarasi wa ndani

Katika kituo cha Dar es Salaam, mkutano pia utaambatana na **maonesho ya Teknolojia, huduma na vifaa vya ujenzi.**

| | |
|---|---|
| Walengwa | Makandarasi, Wataalam washauri; Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wahandisi, Wataalam wanaoshabihiana nao, Waajiri, Watunga sera za uwezeshaji wananchi kiuchumi, watumishi wa taasisi za Serikali zenye dhamana ya manunuzi ya umma katika shughuli za ujenzi na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wanaalikwa kushiriki. |
| Ada ya Ushiriki | Ada ya ushiriki ni **TZS 50,000/=** kwa Makandarasi na **TZS 100,000**/= kwa Wadau wengine. Ada itagharamia mahitaji ya mkutano kama ukumbi, chakula cha mchana na vinywaji.<br><br>Ada ya ushiriki italipwa kwa utaratibu ufuatao:-<br><br>Malipo ya ada ya ushiriki yafanywe benki ya **CRDB Plc** au **NBC ltd**., au **NMB Plc** kwa jina la **CONTRACTORS REGISTRATION BOARD** pia kwa kupitia mitandao ya simu kwa kutumia **"Control Numbers katika vituo husika"** kama ifuatavyo:-<br><br>**Makandarasi**<br><br>**Dar es Salaam:** "Control Number" **995740029791**<br>**Mwanza:** "Control Number" **995740029794** |
| | **Wadau wengine**<br><br>**Dar es Salaam:** "Control Number" **995740029792**<br>**Mwanza:** "Control Number" **995740029795**<br><br>Hakikisha **namba ya simu ya mshiriki** imeoneshwa katika karatasi ya malipo ya benki. |
| Maonesho (Exhibitions) | Bodi inayaalika makampuni na watu binafsi kushiriki kwa kuonesha teknolojia, huduma, bidhaa, vifaa na zana za Ujenzi kwa lengo la kuzitangaza kwa wadau wa sekta ya ujenzi **katika mkutano wa kituo cha Dar es Salaam.** Watakaopenda kushiriki maonesho hayo wawasiliane na **Ndugu Alois Manamba** kwa simu namba **0715809473** au kwa barua pepe kwa anwani almanamba@gmail.com au crbhq@crbtz.org |
| Jinsi ya Kujisajili | Washiriki wathibitishe kuhudhuria mkutano kwa kulipa ada ya ushiriki angalau siku kumi (10) kabla ya tarehe ya mkutano katika kituo husika na kutuma majina na mawasiliano yao katika ofisi yoyote ya **CRB** nchini. **Washiriki wanahimizwa kujisajili mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.** |
| Mafunzo endelevu (PDU) | Washiriki ambao ni wataalam kama Wabunifu majengo, Wakadiriaji majenzi na Wahandisi watakaoshiriki mkutano huu watatuzwa alama **16** za mafunzo endelevu zitatolewa zitakapoombwa katika Bodi zao za usajili. |

Kwa taarifa zaidi fanya mawasiliano kama ifuatavyo:-

CRB Makao makuu, S.L.P 13374 Dar es Salaam Simu 022 213 1169, Tovuti: www.crb.go.tz, Barua pepe: crbhq@crbtz.org CRB Kanda ya Mashariki, S.L.P 33621 Dar es Salaam Simu 022 2771877, Barua pepe: crbez@crbtz.org CRB Kanda ya Ziwa, S.L.P 2815 Mwanza Simu 028 2500218, Barua pepe: crblz@crbtz.org
CRB Kanda ya Kusini, S.L.P 1690 Mbeya Simu 025 2502480, Barua pepe: crbsz@crbtz.org
CRB Kanda ya Kaskazini, S.L.P 16795 Arusha Simu 027 2547107, Barua pepe: crbnz@crbtz.org

# TAHLISO yapewa angalizo kuhusu siasa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

JUMUIYA ya Wanafunzi Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), imepewa angalizo kujiepusha na masuala ya siasa na kujikita katika kutatua kero za wanafunzi.

Angalizo hilo lilitolewa jana na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Prof. Faustine Bee, alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya uwekaji jiwe la msingi katika Ofisi za TAHLISO katika eneo la Iyumbu jijini hapa ambalo ujenzi wake utagharimu Sh. milioni 180.

Prof. Bee alisema jumuiya hiyo inatarajiwa kufanya uchaguzi Mei 23, mwaka huu, wahakikishe wanajikita kutatua kero za wanafunzi badala ya kuigeuza jumuiya hiyo eneo la siasa.

"Viongozi watakaochaguliwa kuhakikisha mnaiga mfano wa Mwenyekiti aliyepita Peter Niboye kwa kujikita kwenye utatuzi wa changamoto zaidi na si kusababisha changamoto zisizo na msingi, mtakaochaguliwa msigeuze TAHLISO kuwa chama cha siasa wala chama cha wafanyakazi bali ibaki na kazi ya kushughulikia changamoto za wanafunzi wenu," alisema.

Aidha, Prof. Bee alisema kuwa kwa kiasi kikubwa kero zinazojitokeza kwenye baadhi ya vyuo husababishwa na baadhi ya viongozi wa wanafunzi wenyewe na si vyuo.

Aliwaasa viongozi wa jumuiya hiyo kutumia vizuri michango wakayopewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi za TAHLISO katika jijini la Dodoma ili likamilike kwa wakati.

Naye Mwenyekiti wa TAHLISO, Peter Niboye, alieleza tangu jumuiya hiyo ianze haijawahi kuwa na kiwanja wala ofisi, lakini chini ya uongozi wake suala hilo limetokea ambapo kwa sasa ujenzi umefikia hatua ya lenta.

Alisema ujenzi huo ulianza Agosti mwaka jana na kwamba umesuasua kutokana na tatizo la fedha kwa kuwa hadi kukamilika kwake inahitajika Sh. milioni 180 na hadi sasa zaidi ya Sh. milioni 26 zimetumika hivyo kuwapo upungufu wa Sh. milioni 155.

**"Viongozi watakaochaguliwa kuhakikisha mnaiga mfano wa Mwenyekiti aliyepita Peter Niboye kwa kujikita kwenye utatuzi wa changamoto zaidi na si kusababisha changamoto zisizo na msingi, mtakaochaguliwa msigeuze TAHLISO kuwa chama cha siasa wala cha wafanyakazi bali ibaki na kazi ya kushughulikia...**

# Ahadi za marais mjadala bungeni

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

MJADALA wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, jana ulitawaliwa na kukumbusha ahadi za marais wanne waliopita na mawaziri wakuu, kuwajengea wananchi barabara kwa kiwango cha lami.

Aidha, wabunge walitaka kuwe na utaratibu wa kukusanya na kufuatilia ahadi zote za viongozi hao, kwa kuwa ipo ahadi ilitolewa tangu mbunge akiwa darasa la tatu na hadi leo haijatekelezwa.

Walitaka mgawanyo sawa wa bajeti kwa kuwa yapo maeneo yamekuwa yakipata fedha nyingi zikajenga barabara, sasa wanaomba za ukarabati na wamepewa, huku maeneo mengine hakuna hata kilomita moja ya kiwango cha lami.

Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM), Abeid Ighondo, alisema akiwa darasa la tatu Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, alitembelea barabara ya Ilongero yenye kilomita 93, na marais waliofuata waliahidi kujenga, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika.

"Alikuja Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuahidi tena kuwa itajengwa, leo naangalia kwenye bajeti naona zimetengwa Sh. milioni 100 za upembuzi yakinifu, tunaomba barabara ijengwe," alisema.

Wakati akichangia, Mbunge wa Jimbo la Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, alisema Jimbo la Ruangwa ambalo mbunge wake ni Waziri Mkuu, kuna barabara tatu za Liwale Ruangwa, Nachingwea Ruangwa hazipitiki, licha ya kutoa ahadi kwingine.

Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga, alitaka wizara kuwa na benki ya ahadi za marais na viongozi wengine kwa kuwa ni nyingi na hazitekelezwi huku akitolea mfano wa ahadi ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ambayo haijatekelezwa hadi sasa.

Mbunge wa Lupembe, Edwin Swalle, alisema bajeti ya mwaka huu haina matumaini kwa kuwa kuna barabara za jimbo hilo ni ahadi za marais waliopita na mawaziri wakuu, lakini hakuna utekelezaji.

"Tuna barabara ya Kibene hadi Madete yenye kilomita 125 tangu enzi za Hayati Benjamini Mkapa, na viongozi wanakwenda wananchi wanawapokea, kuwapigia makofi wanaondoka, lakini wanakaa wanasubiri barabara hawaoni," alisema.

Mbunge wa Mkinga (CCM), Dustan Kitandula, alisema kuna barabara ya Maguk-weni, Maramba, Mtoni Bombo, Korongwe, Ubwa hadi Same ni ahadi ya Rais wa awamu ya tatu, awamu ya nne na tano, lakini viongozi wa dini walishaiomba serikali mbele ya viongozi wa kitaifa ila hadi sasa hakuna utekelezaji.

Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete, alisema hawana barabara ya lami hata kilomita moja, lakini wengine wametengewa fedha nyingi, na kudai kuwa mkoa wa Lindi ni sawa na mikoa mingine.

Mbunge wa Kilombero, Abubakari Asenga, aliomba ridhaa ya Naibu Spika, Dk.Tulia Ackson, akae chini kuonyesha msisitizo, na kabla hajaruhusiwa alikaa chini.

Naibu Spika alimtaka kutokukaa na badala yake ataandaa utaratibu kwa mbunge aliyetaka kupiga sarakasi na mwingine kugalagala wafanye hivyo nje ya ukumbi wa bunge.

Mbunge wa Manonga (CCM), Seif Gulamali, alisema barabara ya Ziba Choma Ndala hadi Puge ni ahadi za marais waliopita, na kwamba ahadi ya mwisho ni ya Hayati Dk. John Magufuli, lakini haijatengewa fedha yoyote.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema kuna barabara ya Lyazumbu hadi Kabwe yenye kilomita 94, ambayo ni ahadi ya Dk. Magufuli, na ipo kwenye ilani ya CCM, lakini hakuna dalili za kuanza na haijatengewa fedha.

Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), Assa Makanika, alisema kuna mbunge ameomba kilomita tatu na hajapewa na kuna aliyeomba kilomita 15 amepewa.

Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavango, alishauri Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), ihamishiwe wizarani ili kuboresha ufanisi wa ujenzi wa barabara.

Mbunge wa Mbinga Mjini (CCM), Jonasi Mbunda, alisema wananchi wa jimbo wamesahaulika kwa kuwa waliahidiwa barabara ya Kitai hadi Litui yenye urefu wa kilomita 9 ya Sh. bilioni 11.5, na alishauliza swali bungeni akaambiwa utaanza mwezi uliopita na hadi sasa hakuna kitu.

Mbunge wa Songwe (CCM) Geoffrey Kasekenya, alisema "Hata sisi tunalipa kodi, lakini hatupewi fedha, keki ya taifa igawanywe mikoa yote kwa usawa."

# Mabomu ya machozi yapigwa wananchi wakitelekeza jeneza

**Na Rose Jacob, MWANZA**

JESHI la Polisi jijini Mwanza limelazimika kutumia nguvu na kuamuru ndugu na majirani kuzika mwili wa kijana Denis Petro (20), anayedaiwa kuuawa na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyambiti, Kata ya Buzuruga wilayani Ilemela jijini Mwanza.

Jana asubuhi wananchi wa Mtaa wa Nyambiti walilazimika kubeba mwili wa marehemu kutoka nyumbani kwao ukiwa kwenye jeneza na kuupeleka ofisi ya serikali ya mtaa kwa madai ya kwamba wamechoshwa na vitendo vya mauaji vinavyofanywa na baadhi ya wenyeviti serikali za mitaa.

Umati wa wananchi uliofurika ofisi za serikali za mtaa ukishinikiza mwili wa marehemu ubaki hapo hadi wapate majibu ya kina kuhusu mauaji hayo, ulitawanywa na polisi waliokuwa na silaha za moto na mabomu ya machozi.

Baada ya polisi kufika kwenye ofisi hizo za serikali, waliubeba mwili wa marehemu ukiwa katika jeneza na kuupeleka Kituo cha Polisi National kisha kwenda kuuzika makaburini.

Katika maziko hayo yaliyofanyika Makaburi ya Nyasaka, polisi waliamuru wananchi kufukua kaburi lililokuwa limefukiwa na kuwataka mwili huo uzikwe chini ya uangalizi wao.

Kazi ya kuzika mwili huo ilifanyika mchana na polisi walihakikisha shughuli yote imemalizika kabla ya hawajaondoka katika eneo la makaburi.

Mwenyekiti anayedaiwa kufanya mauaji hayo, Itare Zeba, anadaiwa kumuua kijana huyo usiku wa mkesha wa sikukuu ya Eid Elftr baada ya kumkamata na kumpeleka ofisini kwake.

Baada ya kutokea mauaji hayo, mwenyekiti huyo anadaiwa kukimbia na kujificha kusikojulikana.

Wakizungumzia tukio hilo juzi wananchi wa mtaa huo wa Miti Mirefu, walisema wamechoshwa na matukio ya mauaji yanayofanywa na baadhi ya wenyeviti wa mitaa.

Hii ni mara ya pili kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa kudaiwa kufanya mauaji ambapo mara ya kwanza Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kishiri jijini Mwanza, alidaiwa kumuua kijana mmoja kwa madai alikuwa kibaka.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Jumanne Muliro, akizungumzia sakata hilo juzi, alisema hajapata taarifa hizo na kwamba akipata undani wake atalifanyia kazi suala hilo.

Aliwataka ndugu wa marehemu kutoa taarifa kituo cha polisi kama wana malalamiko ili walifuatilie.

Hata hivyo, alisema wenyeviti wengi wa serikali za mitaa hawapendwi na watu wanaotenda maovu kwa jamii na kwamba tukio hilo halijatolewa taarifa katika kituo chochote cha polisi.



## HABARI KITAIFA

# Mwinyi: Risasi 728 zilitumika mauaji kiwanda cha sukari

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema mauaji ya watu wanne katika mgomo wa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, ni miongoni mwa vikwazo vilivyoutikisa uongozi wake.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anabainisha mabomo ya machozi 12 na risasi 728 zilizotumika kwenye tukio hilo, lililosababisha kuhamishwa kwa Mkuu wa Mkoa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro.

"Mojawapo ya mambo yaliyoniuma sana kuhusu wafanyakazi mwanzoni mwa uongozi wangu ni kile kilichokuja kuitwa mauaji ya Kilombero. "Mwezi Julai 1986, wafanyakazi kadri ya 500 hivi wa shamba la miwa la Kilombero walifanya mgomo wakidai kuwa wanapunjwa malipo yao.

"Wakagoma kwenda kazini na badala yake wakazingira ofisi na kuwazuia viongozi wa kampuni kuingia ofisini. Katika taftani iliyotokea mawe yakarushwa na kioo cha gari la kiongozi mmoja kikavunjika," anasimulia.

Mwinyi anakumbusha kuwa askari wa FFU walijaribu kutuliza ghasia kwa mabomu ya machozi na walipoona hali haitulii wakatumia risasi na hatimaye watu wanne wakafariki dunia na wengine 16 wakaumia sana.

Anaendelea kusimulia kuwa taarifa zilipoifikia serikali, ilibidi ichukue hatua huku Bunge nalo likitaka hatua zichukuliwe.

"Chanzo chenyewe kilikuwa kutoelewana na tabia iliyodhihirika ya kuwachukulia wakatamiwa kama 'manamba' na kutojali maslahi yao katika hali ya ubinadamu.

"Kwa kawaida ilikuwa kwamba wanapoanza kazi wakitokea makwao wanawekwa kwenye kambi na kukopeshwa fedha kidogo za kununulia panga la kukatia miwa, nguo, chakula na vyombo vya kupikia.

"Mikopo hiyo ilianza kukatwa kutoka kwenye mishahara yao iliyokuwa Sh. 810 kwa mwezi. Mwezi huo wa Julai wakatamiwa wakajikuta wanabaki na Sh. 100 mpaka 200 tu baada ya makato.

"Kwa kawaida walipaswa kulipwa fedha za kufanya kazi nje ya saa za kawaida, pamoja na bonasi. Malipo hayo ndiyo yaliyokuwa yanawawezesha kuishi, lakini kwa mwezi ule wakawa hawakulipwa malipo ya ziada wala bonasi, ndipo wakajikuta wanabaki na Sh. 100 mpaka 200 tu. Wakaamua kugoma," anafafanua. Mwinyi anabainisha kuwa askari waliokuwapo walipoona wanazidiwa, wakaomba waongezwe nguvu na Mkuu wa Mkoa akaidhinisha Kikosi cha FFF kutoka Morogoro kiende kutuliza hali.

Anasema baada ya mauaji hayo, walishauriana ndani ya serikali na hatimaye Waziri wa Kazi akateua tume huru ya uchunguzi ya watu sita, ikiongozwa na Jaji B.D. Chipeta.

"Tume ilipowahoji FFU walijitetea kuwa walipiga risasi za moto baada ya kushindwa kudhibiti hali ile kwa mabomu ya machozi. Aidha, waliona mapanga waliyoshika wakatamiwa na kuamini watawashambulia nayo, hivyo wakapiga risasi kujilinda.

"Wakasema pia kuwa kiongozi wao alijihami ndani ya gari na askari wake walipokosa maelekezo yake, wakarusha risasi kujihami kadri walivyoona inafaa.

"Tume haikuridhika na maelezo hayo maana ulipatikana ushahidi kuwa baadhi ya askari waliwakimbiza wakatamiwa hao mpaka kwenye kambi zao na mmoja wa waliouawa alikuwa amejificha jikoni na mwingine chooni.

"Kuta za kambi zilionesha matundu ya risasi. Ilikadiriwa kiasi cha mabomu ya machozi 12 na risasi 728 zilitumika. Mmoja kati ya waliofariki dunia alikuwa mpita njia," anabainisha. Mwinyi anasema serikali ilipokea na kukubaliana na taarifa ya tume ya Jaji Chipeta na kubaini uongozi wa mkoa wa kisiasa na wa polisi haukutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuifedhehesha serikali kwa matukio hayo ya mauaji.

Anasema tume pia ilibaini udhaifu mkubwa wa uongozi kwenye kampuni ya sukari Kilombero kiutendaji na kisiasa.

"Kampuni ilikuwa shirika la umma, na enzi hizo ilikuwa bado ina tawi la CCM, licha ya tawi la JUWATA (Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania), ambayo nayo kipindi hicho ilikuwa bado jumuiya ya CCM.

"Ilibidi mimi mwenyewe niagize viongozi wa CCM kufanya uchunguzi wa udhaifu wa CCM na JUWATA kiwandani hapo.

"Tulitaka kujua, ilikuwaje wao walikuwapo lakini wakadai hawakuwapo kero na matatizo ya wakatamiwa kiasi cha kuachwa kufuta mpaka yalipolipuka?

"Tume pia ilibaini mazingira magumu sana waliyokuwa wanaishi na kufanya kazi wakatamiwa hao.

"Mmojawapo ya uamuzi wetu kama serikali ikawa kwamba shirika hodhi la sekta ndogo ya sukari (SUDECO), liikopeshe kampuni ya sukari Kilombero Sh. milioni 10 wazitumie kuboresha makazi ya wakatamiwa.

"Pamoja na mambo mengine, tume ya Jaji Chipeta ilituwezesha kufahamu matatizo mengi katika kiwanda hicho na mashamba yake ya miwa.

"Ikabidi tubadili uongozi wote wa juu wa kampuni ya sukari Kilombero na kuwahamishia kwingine waliokuwapo. Tukawahamisha pia Mkuu wa Mkoa na kumpeleka Kigoma na Kamanda wa Polisi wa Mkoa akarejeshwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

# Mbunge alalamikia masharti kwa mabasi

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

MBUNGE wa Gairo, Ahmed Shabiby, ameitaka serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kuzuia mabasi kutoka na abiria kwenye vituo vilivyo nje ya mji.

Alisema vituo vingi vipya vipo mbali na mji na wakati mwingine mwenye gari anaamua kubeba abiria anakamatwa na wanatakiwa kuwashusha ili wachukue usafiri mwingine, jambo ambalo ni mateso kwao.

Alitolea mfano wa kituo kikuu cha mabasi cha Dodoma kilichopo nje ya mji kuwa wanalazimika kushusha abiria na hata kama gari linaelekea mjini.

"Kama mimi mwenye basi nimeamua kumchukua abiria kumpeleka anakotaka wewe kinakuuma nini, wewe ambaye huna hata basi?" Alihoji.

Mbunge huyo alisema kuwa utaratibu huo unatesa abiria wengi na kwamba ni muhimu serikali ikaangalia.

Aidha, alisema kuna kituo kingine Manispaa ya Iringa ambacho kipo umbali wa kilomita 21 na kingine cha Songea umbali wa kilomita 25 kutoka mjini, jambo linalowatesa abiria wengi. Pia aliitaka serikali kupitia upya utaratibu wa malipo ya tiketi kwa kuwa wafanyabiashara wanateseka, kwa kuwa fedha zinachukua muda mrefu kurudi kwao.

Alisema mfanyabiashara anakwenda benki na kupewa taarifa za miezi anapopiga hesabu anagundua kuna fedha nyingi hazijaingia, huku akitolea mfano wa mfanyabiashara Tanga, ambaye aligundua kuna upungufu wa Sh. milioni 23.



Muuguzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto Chanika Dar es Salaam, Brighter Chialo akimpima uzito mtoto mchanga wakati wa uhakiki wa mizani uliofanywa na Wakala wa Vipimo nchini (WMA), jana. Kulia ni Ofisa Vipimo Mkuu wa wakala, Gaspar Matiku. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mkuranga wahadharishwa kuonekana simba wawili

**Na Julieth Mkireri, MKURANGA**

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Alberto Sanga, ametoa wito kwa wakazi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari kutokana na taarifa za kuonekana kwa simba wawili.

Sanga alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na taasisi husika imeanza kufuatilia taarifa za uwapo wa simba hao katika maeneo ya wilaya hiyo na kujiridhisha.

Mkuu huyo alikiri kupata taarifa za kuonekana kwa simba wawili katika wilaya hiyo na kwamba kwa sasa wanafuatilia na baada ya kupata taarifa kamili watatoa kwenye vyombo vya habari na nini kifanyike.

Sanga alisema tahadhari zinatakiwa kuchukuliwa katika maeneo yote ya msitu wa Hifadhi ya Pugu Kazimzumbwi ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku watu wasiingie ndani kufanya shughuli zozote.

Muhifadhi misitu wilayani Mkuranga Charles Kaselya, amekiri kupata taarifa hizo na kusema kuwa wameelezwa na wananchi kadhaa waliokuwa wakisafiri jana na ambao walikua wakivua samaki jirani na msitu eneo la Mwanambaya.

Alisema kuwapo kwa hifadhi za misitu zinazozunguka Wilaya ya Mkuranga ikiwamo msitu wa Pugu Kazimzumbwi, wanyama mbalimbali wamekuwa wakijitokeza katika wilaya hiyo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha mgawanyo sawa keki ya taifa kipewe kipaumbele

MGAWANYO sawa wa keki ya taifa (bajeti), ni kilio cha wabunge wengi, huku wakitoa mifano ya barabara ambazo ni ahadi za marais wanne, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika.

Pia wapo waliosema kuna barabara katika bajeti ziliopita fedha zilitengwa, lakini mwaka huu fedha zimepunguzwa.

Aidha, kila aliyepaza sauti alitoa uthibitisho wa barabara husika kuwekwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa miaka mingi, na nyingine kutoonekana kwenye bajeti.

Keki ya mwaka huu inayogombewa na wabunge ni Sh. trilioni 3.747 ikijumuisha mishahara, matumizi mengine, viwanja vya ndege na upanuzi wa bandari.

Kwa ujumla wachangiaji wote wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, walijikita katika siala la fedha za kukamilisha miradi ya barabara za kuunganisha mikoa, wilaya na maeneo mengine ya shughuli za kiuchumi.

Wapo ambao walionyesha kushangazwa na baadhi ya barabara kuanza kufumuliwa ndani ya muda mfuko, huku nyingine zikiharibika kiasi cha kutengewa fedha za ukarabati ili hali kuna majimbo hawajatengewa hata kilomita moja ya kiwango cha lami.

Wengi waligusia mgawanyo sawa wa keki ya taifa, kwa kubainisha kuwa kuna maeneo yanapewa zaidi na mengine yananyimwa, jambo ambalo siyo sawa.

Wapo walioshauri ni vyema serikali ikajiwekea malengo ya kujenga barabara 50 kwa kila bajeti kuliko kupanga 200, lakini baadaye kushindwa kufikia hata robo ya lengo, jambo ambalo linawakatisha tamaa wananchi.

Wengine walitaka fedha zinazotengwa zitolewa zote kwa wakati mmoja, na kutolea mfano kati ya Sh. trilioni 1 za mwaka jana zilitoka Sh. bilioni 900 na Sh. bilioni 600 hazikutoka.

Kilio cha wabunge hawa ni kikubwa na ni muhimu sana, hivyo ni vizuri serikali ikapitia upya namna inavyogawa rasilimali za nchi, ili kuhakikisha maeneo mengi yanapata huduma sawa hasa miundombinu.


Ni muhimu sana serikali ikatilia maanani malalamiko ya wabunge hasa katika mgawanyo wa keki ya taifa pamoja na kufuatilia kwa karibu ahadi za marais na viongozi wengine, ambazo walizitoa walipowatembelea wananchi hao katika nyakati tofauti.

Ukiwasikiliza wawakilishi hao wa wananchi utabaini kuwa karibu kila jimbo kuna ahadi za viongozi wakuu wa nchi, ambao walizitoa walipopita katika ziara za kikazi au kuomba kura.

Miundombinu ya barabara ni muhimu kwa uchumi wa nchi, kwa kuwa wananchi watakuwa na uhakika wa kuyafikia masoko, na kuendelea kuzalisha waliko (vijijini) kuliko kila mmoja kukimbilia mjini.

Iwapo kutakuwa na miundombinu ya uhakika, maana yake mazao yatafika masokoni na viwandani kwa wakati. Pia kama kuna umeme maana yake wanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani mazao ya wananchi, jambo litakalopunguza wanaokimbilia mijini kwa kuamini ndiko kuna maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi kama hawa ni chukizo kubwa



Na Askofu William Mwamalanga

WANANCHI kushangilia kiongozi anapoondolewa madarakani awe mkuu wa wilaya au mkoa ama taasisi nyingine za serikali kunadhihirisha kuwapo kwa nguvu ya umma.

Aidha, ni udhihirisho kuwa hizo ndizo nguvu walizonazo watu nje ya katiba ambayo haiwapi wananchi haki ya kumwondoa kiongozi anayetenda kinyume.

Ni ushauri wangu kwa mamlaka za uteuzi kuwapa nafasi wenye maadili, uwezo wa kazi na tabia njema.

Ni vyema kuzingatia uadilifu kwani vyeo vinaweza kuwa chanzo cha kukwamisha maendeleo ya wananchi na ukuaji uchumi wa taifa.

Aidha, mamlaka zinazoteua zijiridhishe kwanza kuwa viongozi wanaopewa dhamana wanajibu kero za jamii badala ya kuwa miiba na kuhatarisha ustawi wa taifa.

Mathalani, kwenye mitandao ya kijamii zinatembea taarifa za mkuu wa wilaya anayedaiwa kugeuka 'Adolf Hitler' wa watu na maendeleo yao.

Yanayotokea sasa yanalielekeza taifa kurudi kwenye katiba kwani ya sasa haina nguvu za kumlinda mwananchi dhidi ya viongozi wanaomkandamiza.

Ukirejea maneno ya Baba wa Taifa Julius Nyerere, aliwahi kuonya: 'Katiba tuliyo nayo ikipata kiongozi kichaa watu watapata shida kwelikweli'.

Kwa hiyo ili kuondokana na shida za kundi dogo au viongozi wachache kuwatesa raia wengi ni vyema kuandaa katiba ya wananchi ambayo itaondoa kero za viongozi wabovu ndani ya jamii.

Viongozi wanaotakiwa sasa ni waadilifu, wacha Mungu na siyo wanaokula kiapo cha utii lakini hawathamini umuhimu na majukumu ya uongozi.

Watanzania wanataka viongozi wenye maono ya maendeleo na wachapakazi. Hawapendi wanaoteuliwa kwa malengo ya kisiasa, wakati mwingine kikabila na hata kikanda au kidini.

Yote hayo huhatarisha maendeleo na uchumi na watu.

Wapo viongozi ambao wameleta mabadiliko makubwa kwenye wilaya na mikoa yao waliofanya kazi na hata walipohamishwa wananchi waliandamana kuishinikiza serikali iwarudishe.

Watu waliwalilia kwa kazi kubwa mfano mkoani Mbeya yupo kiongozi aliyebadilisha mkoa huo kiuchumi na kuuwezesha kuzalisha mara dufu kahawa, pareto, ngano maharage na mahindi.

Aidha, alikuwapo mkuu wa wilaya ambaye alipoteuliwa kuwa mkuu wa mkoa wananchi waliiomba serikali ambakize kwenye wilaya yao kutokana na mafanikio makubwa aliyoyafanya.

Kiongozi huyo alianzisha utaratibu kutumia mila kulinda misitu ya asili baadaye utaratibu huo umesambaa na mikoa mingi nchini imeiga.

Kuna viongozi kwa mfano yupo mmoja ambaye wananchi walimbatiza jina la 'mamayetu'. Wanamsifu kuwa hakuwa na makuu na aliufanya mkoa kuongoza kwenye usafi wa mazingira, amani na kila mmoja alifurahi uwepo wake.

**Ni dhahiri mlipuko wa shangwe za wananchi pale anapoondolewa kiongozi wa jinsi hiyo ambaye hakuwasikiliza kwa miaka yote lazima iwe 'sherehe' kwani wanaona kuwa wameutua mzigo wa uonevu.**

Ni wazi kuwa leo viongozi wa serikali wakizuru baadhi ya mikoa watakutana na mabango na maandamano makubwa ya kero za barabara zisizopitika, migomo ya usafiri wa mjini, viongozi kuendeleza siasa za kikabila, wakulima wa baadhi ya vijiji kwa miaka kadhaa wanapiga kelele za kuporwa mashamba, ardhi na wawekezaji 'feki'.

Waporaji ni pamoja na viongozi wanaodaiwa kutumia vyeo vyao kuwapora wananchi kwa kivuli cha uwekezaji huku viongozi wa wilaya na mikoa wakiwa kimya.

Ni dhahiri mlipuko wa shangwe za wananchi pale anapoondolewa kiongozi wa jinsi hiyo ambaye hakuwasikiliza kwa miaka yote lazima iwe 'sherehe' kwani wanaona kuwa wameutua mzigo wa uonevu.

Cha kujifunza kutoka kwa viongozi wanaoshangaliwa walipotumbuliwa, ni funzo kwa walipo madarakani wajihoji kama wanatosha? Iwapo hawatoshi wajisahihishe

Wanaonyanyasa na kutesa wananchi wafahamu kuwa waovu hawana amani. Ila amani ipo kwa wanaoishika sheria kwa mujibu wa zaburi ya 119:165.

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wanaochoma majengo shule kukiona

**Na Rose Jacob, MWANZA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, amelitaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kuwachukulia hatua wanafunzi wanaohujumu miundombinu ya shule kwa kuichoma moto.

Simbachawene alitoa amri hiyo juzi jijini Mwanza, alipofanya ziara ya kikazi yenye lengo la kuimarisha utendaji kazi wa jeshi hilo pamoja na ushiriki wa wananchi katika kujua namna ya kujikinga na majanga ya moto.

Alisema mkoa huo una shida hususani katika masuala ya hujuma kwa kuwa matukio ya moto ni mengi hadi kufikia 93, jambo ambalo siyo sahihi ni lazima kuongezwe juhudi za kuhakikisha yanapungua.

"Matukio ya moto kwenye shule ni utundu wa vijana wanaanza kuhujumu miundombinu kwa sasa na wanafunzi watakaobainika kufanya uharibifu wowote mkubwa wenye madhara katika shule wachukuliwe hatua," alisema Simbachawene.

Aidha, Simbachawene aliwaagiza wakuu wote wa zimamoto nchini kuwaandikia barua ya kuwakumbusha wakurugenzi wa halmashauri na majiji ambao hawajanunua magari ya zimamoto kuyanunua.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa Mkoa wa Mwanza, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto mkoani humo, Ambwene Mwakibete, alisema matukio ya moto na uokoaji kuanzia Julai 2020 hadi Aprili, 2021 yalifikia 93.

Alifafanua kwamba matukio ya moto ni 83 na ya uokoaji 10, vifo 13 na majeruhi 10 na wamefanya uchunguzi wa matukio 10.

Mwakibete alisema katika uchunguzi walibaini vyanzo vya matukio hayo ya moto ni umeme, hujuma na uzembe na kwamba kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama wanaendelea kutoa elimu.

"Tunakabiliwa na changamoto ya visima vya maji ya kuzimia moto, maana mkoa una jumla ya visima 225 na kwamba 66 vinafanya kazi na 159 ni vibovu," alisema.




Mkurugenzi wa Miradi wa Klabu-E Rotary ya Masaki, Akash Shah (watatu kushoto), akikabidhi mashine ya kusaidia kuvuta mtoto wakati wa kujifungua yenye thamani ya Sh. milioni 3 kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mbagala Rangi Tatu, Dk. Mussa Makori, mkoani Dar es Salaam jana, iliyotolewa kwa hisani ya familia ya Gunvantrai na Bhavin Shah. Kushoto ni mwasisi ya klabu hiyo, Vikash Shah, Mkurugenzi wa Utawala wa klabu, Chelsea Lwakatare na wawakilishi wa hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma za kumweka kimada mtoto

**Na Ibrahim Yassin, KYELA**

MUUZA 'yebo yebo' mkazi wa kijiji cha Ipinda Juu, wilayani Kyela, Waziri Mwampondele (35), ametiwa mbaroni kwa tuhuma za kumweka kimada mtoto mwenye umri wa miaka 16 (jina linahifadhiwa), bila kumpa chakula.

Akizungumza jana na mwandishi wa gazeti hili, shuhuda wa tukio hilo, Rafael Katisa, alisema siku mbili zilizopita mke wake alikwenda kuchota maji kwenye kisima kilichopo kwenye nyumba hiyo na kusikia sauti ya msichana ikilia na kuamua kuwaeleza majirani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ipinda, Erick Komba, alisema baada ya kupata taarifa hiyo alimtaarifu ofisa mtendaji wa kijiji.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji huyo, Rozy Mwasabwite, alipofika eneo hilo, alikuta mlango ukiwa wazi bila watu ndani na baadaye alipigiwa simu kuwa mtoto huyo amepatikana maeneo ya barabarani akiwa hoi huku akilalamika kuumwa tumbo.

Alisema, walikwenda kumchukua na kuwapigia simu polisi ambao walifika eneo hilo na kumkimbiza hospitali na kijana huyo alikamatwa na kuwekwa rumande.

Mwenyekiti Komba alisema tukio hilo ni la tatu kutokea katika uongozi wake, tayari watu wawili walihukumiwa kwa makosa ya kulawiti na waliitisha kikao na kuchagua vijana 10 watakaoshiriki katika ulinzi shirikishi na kupita kila nyumba kukagua uhalali wa wapangaji waliopanga katika maeneo hayo.

"Kumekuwa na kawaida kwa watu wengi kupanga vyumba pasipo kufahamika taarifa zao, hii inawaletea shida, kuna uwezekano wakawapangisha wahalifu kwa sababu ya tamaa ya pesa na baadaye ukatokea uhalifu, hatupo tayari kuona matukio ya kinyama na ya kikatili kama haya yanatokea halafu tukae kimya," alisema.

Daktari aliyempokea mtoto huyo kwa matibabu, Jackson Miamvilwa, alisema baada ya kumpima msichana huyo, vipimo vilionyesha kuwa sukari iliisha mwilini kutokana na njaa kwa kuwa hakuwa amekula kwa muda mrefu na pia baada ya vipimo alimkabidhi fomu Mganga Mfawidhi.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Henry Wambua, alisema baada ya vipimo msichana huyo alitibiwa na wazazi wake walimchukua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alikiri jeshi lake kumkamata kijana huyo kwa tuhuma hizo na atapelekwa mahakamani uchunguzi utakapokamilika.

# NMB yawapa fursa vijana wabunifu

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI ya (NMB) imetoa fursa kwa vijana wenye kipaji cha kufanya ubunifu wa mifumo ya kielektroniki inayotumika katika programu zake zenye lengo la kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali kwa wateja wake zinazoendana na mabadiliko ya kielektroniki.

Akizungumza katika hafla ya Wiki ya Ubunifu iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam ambapo NMB ni sehemu ya wadhamini, Mkuu wa Ubunifu na Maendeleo kutoka benki hiyo, Josina Njambi, alisema lengo la kuwa sehemu ya tukio hilo ni kutaka kujivuta karibu zaidi na wadau wanaojihusisha na ubunifu. Alisema benki hiyo imeazimia kufungua fursa zaidi kwa wateja wake kupitia huduma mbalimbali zinazoendana na mabadiliko ya kiteknolojia, lakini ubunifu unaofanyika kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma ikiwamo huduma ya NMB Mkononi.

"Ndiyo maana tulitangaza shindano la kupata vijana watakaokuja na ubunifu wa kipekee kwenye huduma ya NMB App, ambapo tayari tumeshapata vijana 15 watakaoanza kuchuana kwa siku nne ambapo ulianza Mei 18 hadi Mei 2, mwaka huu na mshindi atapata zawadi ya milioni moja.

"Tunachotaka ni kuona kikundi gani kitakuja na utaalamu wa kipekee kwenye ubunifu wa kupata app na huduma zingine za NMB zilizokaa kidijitalii zaidi kwa manufaa ya wateja wetu wapate urahisi zaidi katika kufanya miamala popote walipo na wakati wowote," alieleza Njambi.

Aliongeza kuwa kila siku wanafikiria namna ya kumthamini mteja wao kwa kuwa wabunifu zaidi, ambapo alieleza kuwa ubunifu unasaidia vilevile kuongeza ajira kwa vijana na Watanzania wote kwa ujumla kupitia utoaji huduma.

"Tulipunguza mlolongo wa wateja kupanga foleni kwenye matawi yetu kwa kutoa huduma ya benki kwa simu za mkononi, tulipunguza mlolongo kwenye mashine za kutolea fedha (ATM) kwa kuanzisha NMB Wakala nchi nzima, huu ni ubunifu wa kipekee tuliopata kuufanya," alisema Njambi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) ambayo ndiyo mwasisi wa Wiki ya Ubunifu, Dk. Amos Nungu, alisema awali wazo hilo lilikuwa ndani ya tume hiyo, lakini baadaye wadau wakaamua liwe wazo la nchi nzima kwa kuwa kila kijana wa kitanzania anahitaji kunufaika na ubunifu.

"Tunafahamu kuwa kazi ya serikali ni kuweka mazingira wezeshi, sisi taasisi nyingine tunatakiwa kuzitumia fursa zinazoletwa na serikali kunufaika na kufanya mambo ya kiubunifu hasa katika zama hizi za sayansi na teknolojia," alisema Nungu.

Mkurugenzi wa Programu ya Kusaidia Ubunifu kwa nchi za Ukanda wa Kusini (SAIS), Dk. Flora Tibarazwa, ambaye ni mmoja wa watoa mada alisema ubunifu ni miongoni mwa vyombo vinavyotoa suluhu ya tatizo la ajira duniani na hasa Bara la Afrika.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha jana, wakati wa kuwakaribisha wanahisa wa benki hiyo, katika Mkutano Mkuu wa 24 wa Wanahisa utakaofanyika Mei 22, mwaka huu. Kushoto ni Katibu wa Benki ya CRDB, John Rugambo na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki hiyo, Tully Mwambapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilombero kuzalisha tani 144,000 za sukari

**Na Gwamaka Alipipi**

KIWANDA cha sukari Kilombero kinatarajiwa kufanyiwa upanuzi utakaogharimu Sh. bilioni 571.6, lengo kuu likiwa ni kuongeza uzalishaji wa sukari kufikia tani 144,000 kwa mwaka.

Kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha sukari tani 127,000 kwa mwaka, kupanuliwa kwake kutaongeza uzalishaji hadi tani 271,000 ifikapo mwaka 2023.

Awamu za ujenzi wa mradi unatarajiwa kuchukua miezi 25, na unatarajiwa kukamilika Julai, 2023.

Taarifa iliyotolewa jana na uongozi wa kiwanda hicho, ukimnukuu Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Balozi Ami Mpungwe, ilileza kuwa sababu za kuidhinishwa kwa mradi wa upanuzi wa kiwanda hicho ni pamoja na matarajio ya ongezeko la usambazaji wa miwa kutoka kwa wakulima wadogo wa Bonde la Kilombero kutoka tani 600,000 za hivi sasa hadi tani 1,700,000.

Alisema mradi huo pia utahusisha ujenzi wa vifaa vya ziada vya kuhifadhia sukari na vifungashio ili kupunguza gharama na kuongeza uwezo wa kampuni kuchapa vifungashio vyake.

Balozi Mpungwe alieleza mradi huo utawezesha uzalishaji wa umeme kwa ajili ya matumizi ya kiwanda, kuelekeza umeme wa ziada kwenye gridi ya taifa pamoja na kuboresha ufanisi hasa kwenye gharama kubwa za uzalishaji.

Taarifa hiyo ilieleza: "Wakulima wa miwa wa Kilombero watakuwa wanufaika wakuu kwani ongezeko kubwa la usindikaji wa miwa utahitajika kuendesha kiwanda baada ya upanuzi."

Ilieleza: "Dhamira kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kujenga mazingira wezeshi ya ukuaji wa kasi wa sekta binafsi, yanayodhihirishwa na hatua za makusudi za kulinda viwanda vya ndani vya sukari hapa nchini, yamewezesha maamuzi ya wanahisa kuidhinisha mradi huu wa mageuzi nchini." Mbali na hilo, taarifa hiyo ilieleza kuwa faida za ndani katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huo zinatarajiwa kuwa pamoja na ongezeko la kiwango cha miwa kutoka kwa wakulima wa nje litaongeza mara tatu kipato cha wakulima hao hadi kufikia Sh. bilioni 278 ifikapo mwaka 2028.

Pia idadi ya wakulima wadogo wa miwa itaongezeka kutoka 7,500 hadi wakulima 16,000, hivyo kunufaisha moja kwa moja wakazi zaidi ya 50,000 wanaoishi katika bonde la Kilombero linalozungukwa shughuli za uzalishaji wa sukari.

Balozi Mpungwe alisema pia kutakuwa na ongezeko la ajira ya moja kwa moja ya zaidi ya watu 2,000 kiwandani na katika eneo la kilimo cha miwa.

Alisema kodi ya Sh. bilioni 66.8 zinazolipwa sasa na Kampuni ya Sukari Kilombero inatarajiwa kuongezeka mara tatu kutokana na upanuzi na ufanisi wa biashara ifikapo mwaka 2028.

Aidha, alisema inatazamiwa kuwa mchango wa Kampuni ya Sukari Kilombero kwa uchumi wa nchi utaongezeka kutoka Sh. bilioni 340 za sasa kwa mwaka mpaka wastani wa Sh. bilioni 750. Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kinamilikiwa na Kampuni ya Illovo Sugar kwa asilimia 75 huku serikali ikimiliki asilimia 25.

# Morogoro kutokomeza ugonjwa wa upofu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SHIRIKA la Kimataifa la Sightsavers kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Morogoro, imeanza mpango wa kutokomeza upofu na utoaji wa huduma ya urekebishaji wa vikope kwa wagonjwa katika halmashauri za wilaya ya Morogoro na Gairo.

Utekelezaji wa mpango huo unaofadhaliwa na Sightsavers, ulioanza Mei, mwaka huu (2021), unatarajia kufikia tamati Januari 2023 na kuanza na zaidi ya watu 900 waliobainika na ugonjwa huo, kiasi cha Sh. milioni 328 kimetengwa.

Meneja wa mradi wa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele na msimamizi wa mradi wa kutokomeza vikope kupitia programu ya Step Safe, Peter Kivumbi, alisema uzinduzi wa utekelezaji wa mpango huo ulifanyika Morogoro.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alizindua mpango huo na kukabidhiwa vifaa tiba na dawa vitakavyotumika katika uchunguzi na upasuaji wa macho kwa waathirika wa ugonjwa wa vikope wilaya za Morogoro na Gairo.

Kivumbi alisema, mpango huo utawahudumia watu wote wakataobainika na ugonjwa wa vikope kwenye wilaya hizo.

"Mpango huu unatokana na utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mwaka 2018 ambapo ulibaini kugundulika kwa wangonjwa 353, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na wagonjwa 548 Wilaya ya Gairo na leo ni mwaka 2021 huenda wingine wameongezeka," alisema Kivumbi.

Naye Mkurugenzi mkazi wa Sightsavers hapa nchini, Godwin Kabalika, alisema wamejipanga kuendeleza mradi huo ulianzishwa licha ya rasilimali fedha kidogo inayopatikana.

Alisema, Shirika litaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali na serikali ya mkoa huo kwa kufanya kila liwezekanalo ili kutokomeza upofu.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Kalobelo, alitoa rai kwa wananchi na viongozi watakaoshiriki kutoa matibabu ya ugonjwa wa vikope kushirikisha viongozi wa maeneo husika.

Mhandisi Kalobelo alisema, ushirikishaji kwa viongozi wa maeneo husika wakiwamo wenyeviti wa vijiji, vitongozi na viongozi wa kaya ni jambo la muhimu ili kupata mafanikio ya utekelezaji wa mradi huo.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuweka mazingira katika hali ya usafi na kutumia majisafi na salama kuepuka wananchi kupatwa na vikope.

# Wanahisa CRDB kuidhinisha maamuzi

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya CRDB, inatarajia kufanya mkutano mkuu wa 26 wa wanahisa ili kujadili masuala mbalimbali ikiwamo kupitisha na kuidhinisha maamuzi kibenki.

Mkutano huo unafanyika mkoani Dar es Salaam, Mei 22, mwaka huu, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Akizungumza jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema ili kutoa fursa kwa wanahisa wengi zaidi kushiriki mkutano huo, utafanyika kidigitali kutoa fursa kwa ambao hawataweza kufika mjini Arusha.

"Kwa kuzingatia uzoefu tulioupata kwa kufanya mkutano huu kwa njia ya mtandao, wanahisa walipitisha pia azimio la mkutano wa 26 kufanyika kwa njia zote mbili kwa maana ya kuruhusu wanahisa wanaoweza kushiriki kwa kufika Arusha pia kuruhusu washiriki kwa njia ya mtandao," alisema Nsekela.

Nsekela alisema mkutano huo, utatanguliwa na semina maalumu kwa wanahisa wake ili kukuza uelewa wa masuala mbalimbali ya fedha na uwekezaji katika masoko ya mitaji.

Alisema mada mbalimbali zitawasilishwa na wataalamu wa masuala ya fedha pamoja na sheria na uwekezaji katika masoko ya mitaji.

Nsekela aliongeza kwamba zaidi ya wanahisa 1400 waliweza kushiriki mkutano wa mwaka jana, idadi ambayo haijawahi kufikiwa katika mikutano ya kawaida ambayo hufanyika jijini Arusha kwa miaka yote.

"Nachukua fursa hii kuwakaribisha wanahisa wote katika semina na mkutano mkuu na niwahakikishie wanahisa wote ambao watashiriki kwa njia ya mtandao," aliongeza Nsekela.

Aliongeza kuwa na mambo mengine yatakayojadiliwa katika mkutano mkuu huo, ikiwamo maboresho ya katiba ya kampuni, shauku kubwa kwa wanahisa ni kufahamu juu ya pendekezo la gawio kwa wanahisa kwa mwaka uliopita.

"Ukizingatia kuwa CRDB imeendelea kupata matokeo mazuri sokoni katika hesabu za mwaka wa fedha ulioisha benki ilipata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 236, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15 kutoka Sh. bilioni 175 iliyopatikana mwaka 2019."

## DC awaasa wauguzi lugha mbaya kwa wagonjwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKUNGA na wauguzi wametakiwa kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa na kutoa huduma stahiki ili kunusuru vifo visivyokuwa vya lazima kwa wajawazito na watoto.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, katika Halmashauri ya Msalala.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo mwaka huu ni 'Wauguzi ni sauti inayoongoza dira ya huduma ya afya'

Macha alisema mwaka 2020 wajawazito sita na watoto 23, walipoteza maisha.

"Idadi hii ya watoto wachanga kupoteza maisha ni kubwa ikilinganishwa na vifo vya wajawazito mna jukumu la kuhakikisha mnatoa elimu ya afya ya uzazi katika vituo vyenu vya kazi ili itambue umuhimu wa huduma za afya ya uzazi," alisema Macha.

Alisema serikali imepanga kuleta wataalamu wa afya na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha wajawazito na watoto wanapata huduma bora.

Kwa upande wake, Muuguzi Mkuu wa halmashauri hiyo, Flora Magembe, alisema wanakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi katika zahanati na vituo vya afya vilivyopo kijijini.

Alisema huko vijijini bado kuna mwamko mdogo wa jamii kuwaruhusu wajawazito kujifungulia katika vituo vya afya ama hospitali.

Aidha, alisema halmashauri hiyo ina wauguzi na wakunga 98 sawa na asilimia 53 ambao hawatoshelezi mahitaji na wanaohitajika ni 85 sawa na asilimia 47.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Flora Sagasaga, alisema wanaendelea kutatua kero mbalimbali zinazowakabili watumishi wa sekta ya afya ikiwamo kuwapa motisha watumishi wanaofanya kazi vizuri, kuwalipa stahiki zao za likizo na kuwapandisha madaraja.

**Kwa upande wake, Muuguzi Mkuu wa halmashauri hiyo, Flora Magembe, alisema wanakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi katika zahanati na vituo vya afya vilivyopo kijijini.**

# Bunda yakabiliwa upungufu wa wauguzi na waganga

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

IDARA ya Afya katika Halmashauri ya Mji wa Bunda mkoani Mara, inakabiliwa na upungufu wa wauguzi na waganga na kusababisha wafanye kazi hadi saa za ziada.

Wauguzi hao walitoa malalamiko yao jana kupitia risala waliyoisoma kwenye maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, iliyofanyika katika viwanja vya kituo cha afya Bunda, mjini Bunda.

Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi (TANNA), Violet Juma, akisoma risala hiyo, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo ya upungufu wa wauguzi, baadhi ya vituo vya afya kuongozwa na wauguzi hali inayosababisha kuzidiwa na kazi na kufanya majukumu yaliyo nje ya taaluma yao.

Walisema kuwa kutokana na hali hiyo muuguzi ndiye anayegeuka kuwa mganga mfawidhi wa kituo, mfamasia na mhasibu na kwamba licha ya kufanya majukumu yote hayo hawalipwi stahiki zao, wala kupandishwa madaraja ambayo ni haki yao.

"Pamoja na uchache wetu bado tuliweza kustahimili kutoa huduma thabiti katika kipindi chote cha mlipuko wa janga la corona kwa saa 24 katika mazingira magumu," walisema katika risala yao.

Pia walisema wanaadhimisha siku hiyo ikiwa ni hatua ya kumuenzi mwasisi wa taaluma ya uuguzi na ukunga duniani Florence Nightngale kwa mchango wake mkubwa.

"Tunaiadhimisha siku hii kama kumbukumbuku muhimu ya kumuenzi mwasisi wa taaluma ya uuguzi na ukunga kutokana na kuwa mtu pekee duniani kugundua namna bora ya kupunguza vifo vilivyotokana na majeruhi waliokuwa wakipigana vita enzi za ukoloni kwa kuwasafisha vidonda ili kuzuia maambukizi ya wagonjwa."

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Janeth Mayanja, alisema changamoto hizo wamezichukua na zitafanyiwa kazi kwa kushirikiana na wizara husika na serikali, pia aliwapongeza wauguzi hao kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhudumia watu, kwa ajili ya kuokoa maisha yao.

Hata hivyo, aliwaonya wauguzi wenye tabia ya kuiba dawa za serikali na kuziuza, kuwa wakikamatwa watashtakiwa kwa kosa la uhujumu uchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, na mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ambaye alikuwa ni mwenyekiti wa halmashauri ya mji wa Bunda, Michael Kweka, waliwapongeza wauguzi wote kwa kufanya kazi ya kuhudumia wana nchi.

Kaulimbiu ya siku ya wauguzi duniani mwaka huu, ni wauguzi sauti inayoongoza dira ya huduma ya afya.



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (kushoto), akizungumza na waumini wa duni ya kiislam katika msikiti wa kijiji cha Bukima jimboni humo juzi, baada ya kuwapa mkono wa Idd na kuhimiza wananchi kushiriki katika shughuli za kijamii kwa ajili ya kujiletea maendeleo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijiji 80 kunufaika umeme wa REA

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

JUMLA ya vijiji 80 Wilaya ya Morogoro vinatarajiwa kunufaika na mradi wa umeme wa REA awamu ya tatu baada ya serikali kuviorodhesha kuingia kwenye mpango huo.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wilaya ya Morogoro, Hilda Luvuvu, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Morogoro.

Hilda alisema vijiji ambavyo havina umeme katika wilaya ni 80 na tayari maandalizi ya kupeleka umeme yameshaanza, muda wowote vitakuwa na nishati hiyo.

Alisema wataalamu wa umeme huo wameshaanza hatua za awali za kuvikagua na baada ya kukamilika kwa kazi hiyo vijiji vyote 150 vitakuwa na huduma hiyo na kuchochea maendeleo.

"Zoezi la kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo havina huduma hii ya nishati linakwenda vizuri na muda wowote kuanzia sasa vijiji vyote 150 katika halmashauri ya wilaya ya Morogoro vitakuwa na umeme wa REA," alisema Hilda.

Alisema kuwapo kwa umeme huo katika wilaya hiyo kutachochea ukuaji wa uchumi kwa wananchi na TANESCO itahakikisha kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo hajipata umeme linafanyika kwa haraka zaidi.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Lucas Lemomo, alisema wananchi wa vijiji hivyo wapo tayari kuona umeme huo unawafikia kwa kuwa wanaamni itakuwa ni moja ya njia ya kupata maendeleo.

Alisema kuwapo kwa umeme wa REA katika vijiji vyote, halmashauri yake itakuwa ma maendeleo mengi ya kiuchumi kwa kuwa watu wengi watavutiwa kufika katika wilaya hiyo kwa ajili ya kuwezeka viwanda vingi.

"Wilaya yetu hii ni maarufu kwa kilimo cha mazao ya aina mbalimbali hivyo kitendo cha kuwa na umeme kutasaidia kuwavuta wawekezaji kuja hapa kwa ajili ya kuwekeza viwanda vya uchakataji wa mazao ya wakulima," alisema Lemomo.

Pia alisema kitendo cha uchakataji wa mazao kitaongeza thamani yake na kufanya uchumi wa wakulima ambao ndiyo walishaji wakubwa wa mazao hayo kuwa imara na pia kutasaidia kuongeza mapato ya halmashauri hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, Rehema Bwasi, aliwataka wananchi wote kuepuka kuwa chanzo cha kukwamisha mradi huo kwa kuwa utakuwa chachu kubwa ya maendeleo kwa kila kijiji.

# Mradi wa miundombinu watekelezwa h/shauri 45

BUNGE limeelezwa kuwa majadiliano ya utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji Miundombinu katika Miji (TACTIC),unaotarajiwa kutekelezwa katika Halmashauri za miji 45 nchini yamekamilika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Dodoma Mjini (CCM), Anthony Mavunde.

Katiba swali lake, Mavunde, alisema mradi huo unagusa Jiji la Dodoma na wataalamu walishakaa na kuibua miradi hiyo na kuhoji lini Wizara hiyo na Wizara ya Fedha zitakaa kukwamua vikwazo vilivyopo ili wananchi wanufaike na mradi huo.

Akijibu, Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alisema mradi huo ni wa kimkakati na serikali ya awamu ya sita imeweka mradi huo kuwa wa kielelezo katika kujenga miundombinu ya barabara, masoko na madampo.

"Mei 10, mwaka huu nilikaa mimi na Waziri wa Fedha Mwigulu Nchemba na wataalamu wetu, na tukakubaliana majadiliano yamekamilika na sasa yanapelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya taratibu za kusaini mkataba wa kuanza ujenzi huu," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo ni muhimu kwa Jiji la Mbeya, Arusha, Dodoma, Mwanza na Tanga.

"Mradi huu naubeba kama mradi wangu maana kutopatikana kwake sitaweza kurudi bungeni lakini na kwa miji yote 45 tutahakikisha tunaanza utekelezaji mara moja," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Nyamagana (CCM), Stanslaus Mabula, alihoji ni lini serikali itakuwa tayari kuanza mradi wa TACTIC ili kufikia Malengo Makuu ya Serikali ya mwaka 2020 - 2025 katika kuboresha miundombinu ya barabara.

Akijibu, Naibu Waziri David Silinde, alisema mradi unatarajiwa kutekelezwa na Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Aidha, alisema serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kuhusu upatikanaji wa fedha hizo na mradi utaanza kutekelezwa baada ya kukamilika kwa majadiliano na fedha kutolewa.

## Mbunge ataka maji kutoka Mto Kwedibuluma

MBUNGE wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, ametaka serikali ianze mkakati wa kusambaza maji kutoka Mto Kwedibuluma katika kata za Wilaya ya Mvomero na Kilindi.

Akiuliza swali bungeni jana, Kigua alihoji serikali itaanza lini kusambaza maji hayo kata ya Kibati Wilaya ya Mvomero na kuyasambaza katika kata ya Tunguli,Kwekivu,Masagalu na Songe wilayani Kilindi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema serikali ina mpango wa muda mrefu wa kutekeleza mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha mto Diburuma kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

"Hatua iliyofikiwa ni kufanyika kwa utafiti wa ubora na uwingi wa maji katika chanzo hicho ili kujiridhisha na kiwango cha maji kwa ajili ya kunufaisha vijiji vilivyopo kwenye kata nne za Tunguli, Kwekivu, Masagalu na Songe," alisema.

Alisema utafiti huo utakamilika kabla ya mwezi Juni, 2021 na takwimu zitakazopatikana zitatumika kufanya usanifu wa kina wa mradi huu.

"Kwa sasa kata za Tunguli, Kwekivu, Masagalu na Songe zinapata huduma ya maji safi na salama kupitia visima virefu vitano na visima vifupi 15,kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma ya maji katika kata hizo na Halmashauri ya Kilindi kwa ujumla, katika mwaka wa fedha 2021/22," alisema.

Aidha, alisema serikali imetenga kiasi cha Sh.bilioni 2.14 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.



Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Omari Kigua, akizungumza Bungeni, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Wakopaji matrekta kuongezewa mikataba

WIZARA ya Viwanda na Biashara, imesema serikali inafanya utaratibu wa kuwapa mikataba ya nyongeza wakopaji wote wa matrekta ya URSUS nchi nzima.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe, alibainisha mpango huo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kiteto (CCM), Edward Olelekaita.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango wa kupunguza bei na kuongeza muda wa mkopo wa Matrekta waliokopeshwa wakulima wa Jimbo la Kiteto na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Akijibu, Naibu Waziri huyo alisema: "Mikataba ya nyongeza inahusisha bakaa ya deni na haitozwi riba, utaratibu wa kupewa mikataba ya nyongeza unahusisha mkulima na NDC kukaa pamoja na kufanya majadiliano ya namna mkulima atakavyolipa deni lililobaki."

Alisema zoezi hilo pia limeshaanza kwa wakulima wa Kiteto katika kipindi hiki na linaaendelea ili kuwafikia wale wote ambao muda wa mikataba yao umepita.

Awali, alifafanua kuwa mradi wa Matrekta wa URSUS unatokana na Mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi baina ya Serikali ya Tanzania na Serik 28,ali ya Jamhuri ya Poland, uliosainiwa Septemba 28, 2015.

"Serikali ya Jamhuri ya Poland iliiteua kampuni ya URSUS na Serikali ya Tanzania iliiteua SUMA JKT kama watekelezaji na baadae mradi huu ukahamishiwa Shirika la la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa utekelezaji," alisema.

Hata hivyo, alisema katika mkataba huo, Serikali ya Uholanzi ilitoa Mkopo nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 110 kwa riba ya asilimia 0.3 kwa mwaka, ukiwa na kipindi cha mpito cha miaka mitano na utarudishwa katika kipindi cha miaka 30.

"Lengo la mkopo huo ni kugharamia maendeleo ya sekta ya kilimo nchini," alisema.

Kuhusu kupunguza bei, alisema kabla ya kupanga bei ya matrekta, Serikali kupitia NDC, ilifanya uchambuzi wa gharama na kupanga bei kulingana na uchambuzi huo.

"Bei hizi zilipangwa kwa kuzingatia gharama za uagizaji, kutolea bandarini, kuunganisha na gharama zingine za usimamizi," alisema.

Aidha, alisema serikali ilipanga bei nafuu ambayo wakulima wengi wanaweza kununua na kukopa matrekta hayo kutokana na mchango wake katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na kuzalisha malighafi za viwandani.

"Ili kurahisisha uuzaji wa matrekta hayo, mkopo uliotolewa haukuwa na riba. Lengo kuu la Serikali sio kupata faida bali kuwawezesha wakulima kujikwamua kutoka kwenye matumizi ya jembe la mkono na kuongeza tija zaidi," alisema.

Alisema hivyo bei ya matrekta hayo kwa sasa inarejesha gharama za matrekta hayo pekee bila kupata faida.

"Katika kurahisisha ulipaji wa mkopo kwa wakulima, kuanzia mwaka 2020, Serikali kupitia NDC iliongeza muda wa kulipa mikopo kwa wakopaji ambao muda wa mikataba yao imeisha," alisema.



Ukurasa 13

## Uteuzi wa Queen Sendiga RC Iringa....



Ukurasa 14



# MILTON OBOTE Rais aliyeacha historia ya kupinduliwa, akarejea Ikulu

siasa

JUMATANO MEI 19, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

UCHAMBUZI

# RAZA atoa ya moyoni

- Ataka maridhiano, majadiliano
- Tume ya Fedha za Muungano



Mohamed Raza akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya ukimya wa muda mrefu, mwakilishi wa zamani wa Jimbo la Uzini visiwani Zanzibar, Mohamed Raza, ameibuka na kutoa ya moyoni akisisitiza kuwa haiwezekani kuongoza nchi bila kuwa na majadiliano na maridhiano.

Raza anayeyafananisha mambo hayo na mkombozi, anaishauri serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan na ya Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuendeleza majadiliano, maridhiano na kuwa wakweli katika utendaji.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe jijini Dar-es- Salaam, kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa na kijamii anasema, Tanzania inahitaji uongozi unaotetea haki, wenye hofu ya Mungu na unaoendeleza majadiliano na maridhiano kila wakati yanapohitajika.

Raza alikuwa mwakilishi wa Uzini, lakini akaondolewa kwenye nafasi hiyo, kwa kile alichokiita 'figisu figisu' wakati wa kura za maoni kwenye uteuzi wa wagombea mwaka 2020, anaanza na suala la Muungano.

Anasema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni mzuri lakini ili uendelee kuwa imara ni lazima Watanzania wavumiliane, kuheshimiana na kujadiliana.

Aidha, zipo kero za Muungano ambazo zinatatulika kwa kuunda Tume ya Pamoja ya Muungano kama inavyoelezwa kwenye katiba.

Ibara ya 134 (1) ya katiba, inaelekeza kuundwa Tume ya Pamoja ya Fedha yenye wajumbe wasiozidi saba wanaoteuliwa na Rais na inayataja majukumu yake kuwa ni kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila serikali.

Kadhalika inachunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na uhusiano wa masuala ya kifedha baina ya serikali mbili, kwa mujibu wa katiba itatekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia au kuiagiza.

Anamshauri Rais Samia Suluhu Hassan, kuteua wajumbe na kuunda Tume ya Pamoja ya Fedha za Muungano.

"Hii ipo kikatiba. Ibara ya 134 inaagiza kuundwa tume hiyo itakayosimamia fedha zinazohusu masuala ya Muungano. Lakini hili halijafanyika. Naomba Rais Samia ateua wajumbe hao na kazi iendelee," anasema Raza.

Raza ambaye ni mfanyabiashara visiwani humo, anasema katiba imeona umuhimu wa chombo hicho kushughulikia masuala ya mgawanyo wa fedha za Muungano, kufuatilia mwenendo wa uchumi na kwamba uwepo wa tume hiyo ni muhimu ili maamuzi yafanyike kwa misingi ya sheria na maelekezo ya katiba.

"Kuwa na tume hiyo na pia kuwapo Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia na Muungano ni wazi kero zitamalizika. Niseme Muungano wetu ni imara na kama kuna asiyeutaka aondoke." Anasema.

**MUUNDO WA SERIKALI**

Akizungumzia muundo wa serikali ndani ya Muungano kama kuna tatizo, anasema mambo yalivyo serikali zimekamilika na hata ukiangalia kuna serikali ya Tanzania ambayo Bunge la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma linazungumzia bajeti na masuala ya Tanzania Bara.

Kadhalika, Raza anasema kuna kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachofanyika Zanzibar kikijadili bajeti na masuala ya Zanzibar na hakuna suala jingine zaidi.

Anakumbusha kuwa mambo ya Muungano yapo kwenye Wizara za Ulinzi, Fedha, Mambo ya Ndani na ile ya Ushirikiano wa Kimataifa.

Anasema msimamo wake ni kuunga mkono Muungano uliopo na kwamba Tanzania Bara na Zanzibar ni nchi huru na kila upande una wajibu wa kuulinda na kutetea umoja na mtangamano.

Hata hivyo, anawashauri viongozi kufanya uchunguzi na kufuatiliaji kwa kina kabla ya kufanya maamuzi na kwamba kiongozi anapoletewa taarifa kuhusu mtu fulani au jambo lolote linalohusu serikali, Muungano au taasisi yoyote asichukue maamuzi bila kuchunguza na kuujua ukweli.

"Akamilishe kwa kufanya maamuzi kwa hekima na haki kwa sababu zama hizo yatasemwa mengi." Anasema Raza.

**SERIKALI Vs CORONA**

Raza anasema Rais Samia ameanza kazi kwa kutafuta ukweli, kujadiliana na hachukua hatua dhidi ya corona bila kushirikisha wataalamu.

"Ameanza na kusikiliza ushauri wa wataalamu, na kuunda kamati ya kuishauri serikali masuala ya corona. Nampongeza ameunda kamati kwa sababu suala la COVID -19 ni gumu pengine utafika wakati mataifa yanakuwa na msimamo mmoja kama hujachanja usivuke mipaka."

Anasema, mathalani chanjo ya homa ya manjano ni makubaliano yanayoonekana leo ya kudhibiti magonjwa na kuna nchi ambazo huruhusiwi kuingia kama huna kadi ya chanjo ya homa ya manjano (yellow card).

Anasema baadhi ya mataifa hayo ni pamoja na Singapore, China, India na kwamba suala la Tanzania kukaa kimya kwenye co-

INAENDELEA UK. 12



Makamu wa Rais wa SUK Zanzibar, Othman Masoud Sharif, katika kazi zake. **PICHA: MTANDAO**

# MOTO WA SUK

## ■Umoja wairudisha Zanzibar ya 'zamani'
## ■Shauku ni kuona mafisadi wakishtakiwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

APRILI mwaka huu Tanzania imeadhimisha miaka 57 ya Muungano, wakati hayo yanatokea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), inaendelea kuwa na muundo wa umoja wa kitaifa (SUK), Wazanzibari wakiona kuwa ni jambo la kujivunia kuwaunganisha wananchi na kutumia juhudi zote ili kuzika na kusahau tofauti zao.

Serikali ya Rais Hussein Ali Mwinyi, inaelezwa kuwa imeanza kwa mafanikio katika jitihada za kuondoa mitazamo ya chuki na ubaguzi unaotokana na tofauti za kiitikadi na kisiasa.

Kutoshirikiana, watu kugawanyika huku wakitazamana kwa macho ya uhasama na dharau kunaelekea kubakia historia baada ya maafikiano ya viongozi wa kisiasa kufuatia mwafaka wa kisiasa uliofikiwa chini ya Rais mstaafu Amani Abeid Karume na aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad (marehemu) mwaka 2009.

Wana Unguja na Pemba wanasahau yaliopita huko nyuma tangu 'mazonge' ya uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi vya siasa wa mwaka 1995 hadi wa mwaka 2020 na sasa wakijadili zaidi maendeleo kuliko siasa na vyama.

Kwa mara ya kwanza SUK imeshirikisha Chama cha ACT-Wazalendo baada ya CUF kukumbwa na mgogoro wa uongozi kati ya Mwenyekiti Profesa Haruna Lipumba na aliyekuwa Katibu Mkuu Maalim Seif.

Pamoja na hayo, uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kudaiwa kuwa na kasoro kadhaa ACT- Wazalendo ilipata majimbo mawili ya ubunge Pemba na manne ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kabla ya kupata nyongeza ya wajumbe wawili wa kuteuliwa.

Kuundwa SUK na kampeni za Rais Hussein Mwinyi zilionyesha kuwa haikuwa kazi ngumu kwake kurejesha umoja na mshikamano kwa sababu wananchi walimwamini na kujenga matumaini naye kabla na baada ya kushika urais.

Akitumia kauli mbiu: "Yajayo yanafurahisha pamoja na yajayo neema tupu' ameyavutia makundi ya wanawake, vijana na wazee na sasa siasa za chuki na ubaguzi zimezikwa.

Bila ya kujali tofauti za itikadi za kisiasa wafuasi na wanachama wa vyama tofauti wanaweza kukaa pamoja kwenye maskani au barazani kubadilishana mawazo au kunywa kahawa pamoja, kushirikiana katika shughuli za kijamii tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Akizindua Baraza la Wawakilishi (BLW) mwaka jana, Rais Hussein Ali Mwinyi, alisema Wazanzibari wanahitaji kujadili zaidi dhana ya maendeleo kuliko tofauti za kisiasa. Alitaka wajielekeze kwenye historia ya mapinduzi au simulizi za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

> Anasema taasisi za umma zina jukumu la kuwawahudumia wananchi wote kwa usawa, mizani na haki wala si kubagua au kukomoana: "Najua kila mtu hapa ana utamaduni wake na chama chake cha siasa lakini kwangu mimi katika kuwatumikia natanguliza mbele Zanzibar na maslahi ya Wazanzibari wote," anasema Masoud.

Anasema jambo pekee muhimu kwa wananchi ni uwekaji na utekelezaji wa malengo yaliyoleta mapinduzi kwa azma ya kujenga uchumi imara hivyo lazima suala la amani na umoja wa kitaifa lipewe kipaumbele na wananchi pamoja na wanasiasa.

Anaeleza kuwa serikali yake imekusudia kuimarisha misingi ya uwajibikaji, utendaji wenye tija, uwazi serikalini, uaminifu na uadilifu badala ya chuki, ubaguzi, mgawanyiko na uhasama. Pia anawataka watumishi wa umma kupambana na ubadhirifu wa mali za umma, akitaka rushwa na ufisadi vipigwe vita.

"Mimi si kama napenda kufukuza watu kazi. Niliwahi kusema huko nyuma sina nia ya kumtafuta mchawi wala sitafukua makaburi. Lakini inapofikia watu wanapoendelea na ubadhirifu na wizi wa mali za umma sitanyamaza bila kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria. Wapo wanaodhani nimeishiwa nguvu. Wenye fikra hizo nadhani wanajiongopea. Nitapambana na wizi wa aina yoyote hadi wizi utakapokoma. Katika uongozi wangu ndiyo kwanza safari imeanza..." anaonya Rais.

Kwa upande wake Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, anaahidi kuwatumikia wananchi wa Zanzibar bila ya kuangalia itikadi za vyama vyao vya siasa.

Anasema taasisi za umma zina jukumu la kuwawahudumia wananchi wote kwa usawa, mizani na haki wala si kubagua au kukomoana: "Najua kila mtu hapa ana utamaduni wake na chama chake cha siasa lakini kwangu mimi katika kuwatumikia natanguliza mbele Zanzibar na maslahi ya Wazanzibari wote," anasema Masoud.

Suala la kupambana na rushwa na ufisadi linahitaji ujasiri ili kuweza kufikia malengo ya kujenga Zanzibar mpya kwa kuitokomeza rushwa na ubadhirifu ikibaki kuwa historia kama vile siasa za chuki na ubaguzi Zanzibar zilivyopeperushwa na kutoweshwa.

**ANGALIZO MUHIMU**

Wazanzibari wanaendelea kutazama hadi sasa hakuna mtuhumiwa aliyefikishwa mahakamani kwa mashtaka ya rushwa nzito au ufisadi wa mali za umma licha ya kuwapo kashfa lukuki na miradi mibovu ambayo imesababisha hasara kwa serikali.

Hiyo ni pamoja na ununuzi wa meli ya Mapinduzi II, ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, kashfa ya majengo ya Mambo Msiige na Starehe Kilabu, mradi wa ukarabati wa jengo la kihistoria la Beit al Ajab, malipo hewa kwenye vikovi vya SMZ na kuuzwa na kuvunjwa kwa hoteli ya Bwawani.

Suala la viongozi wanaotuhumiwa kutumia madaraka vibaya ikiwamo kupora ardhi kwa manufaa binafsi pia linahitaji kupewa nafasi na serikali ya awamu ya nane ya SUK katika kusimamia misingi ya utawala bora na kuweka usawa mbele ya utawala wa sheria.

# Mohamed Raza atoa ya moyoni

**INATOKA UK. 11**

rona, hivyo kubaki bila ufumbuzi lingeweza kuleta athari kwa wafanyabiashara, safari za kimataifa na hata ushirikiano na nchi nyingine duniani.

Juzi kamati iliwasilisha mapendekezo kwa Rais na kushauri kuwepo na matumizi huru ya chanjo, hatua za dharura za kukabiliana na majanga, kutoa taarifa za corona na kutumia tiba asili kudhibiti ugonjwa huo.

**VIONGOZI WAKWELI**

Raza anataka watu kuwa wakweli, akikumbusha kuwa zama za hadaa zimekwisha na kinachotakiwa ni viongozi wa wazi wanaotenda kazi kwa haki kuanzia viongozi wa CCM, serikali kwa kutekeleza ilani ya chama Tanzania Bara na Zanzibar.

Anakumbusha kuwa uongozi wenye tamaa mara nyingi hautendi haki iwe ndani ya chama, serikali au popote na kuwasifu viongozi wa serikali ya Zanzibar na Tanzania kuwa hawaongozi kwa tamaa, aliyoiita 'ambition'.

Akifafanua zaidi anasema uongozi zama hizi unatakiwa kuongoza na fikra kuwa taifa kwanza kwa sababu ni la kudumu lakini uongozi ni wa muda na unaondoka.

"Nawashauri viongozi wafikirie suala la kuacha alama za kukumbukwa. Wafanye mambo ambayo yatafanya waheshimiwe na kukumbuka. Wafahamu kuwa wanaondoka na Tanzania pamoja na Zanzibar zitabaki." Anasema Raza.

Mwanasiasa huyo anasisitiza ukweli, kumwogopa Mungu na kuwatumikia wananchi kwa upendo na kufahamu kuwa maisha yana mwisho lakini nchi na mataifa yataendelea kuwapo.

***ITAENDELEA WIKI IJAYO***

# Uteuzi wa Queen Sendiga RC Iringa....

## ▪ ADC yakunwa, mguu sawa kutoa tamko



Queen Sendiga, alipokuwa katika moja ya mikutano, kwenye kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana.

**Na Sabato Kasika**

KILE alichoahidi Rais Samia Suluhu Hassan, kukifanya katika uteuzi wa viongozi serikalini kwamba hataangalia itikadi ya yeyote atakayeona ana uwezo wa kusaidia taifa kufikia maendeleo, kimetimia.

Anatimiza ahadi kwa kumteua Naibu Katibu Mkuu wa Alliance for Democratic Change (ADC) Taifa, Queen Sendiga, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa.

Queen aliyepeperusha bendera ya ADC akiwa mgombea urais, kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka jana akiwa ni miongoni mwa wanawake wawili waliojitokeza kutaka nafasi hiyo ya juu, alikuwa pamoja na Cecilia Mwanga, aliyegombea kwa tiketi ya Demokrasia Makini.

NI NINI HATIMA?

Gazeti hili linazungumza na Katibu Mkuu wa chama hicho, Doyo Hassan, kujua kama ADC imeshirikishwa katika uteuzi huo.

Hassan anasema, ADC haikushirikishwa katika mchakato wa uteuzi huo bali inaamini kwamba ahadi aliyoitoa Rais, kwamba hataangalia itikadi ya mtu yeyote atakayeona ana uwezo wa kusaidia taifa lake katika uongozi, inatosha.

"Ninachoweza kukuambia ni kwamba chama kinajiandaa kukutana na kutoa tamko ambalo litamuelezea mwanachama wetu na hatima yake tukihusisha uteuzi huo," anasema Hassan na kuongeza kuwa ADC , itakutana na kutoa tamko la kumtia moyo Queen afanye kazi yake mpya kwa weledi na kwa mafanikio kikiamini kuwa kwa utendaji wake sifa hazitakuwa kwake au serikali pekee bali na kwa ADC pia.

"Tutafanya hivyo, kwa sababu tumefurahi kuona chama chetu kinaendelea kuaminiwa na kutambuliwa kutokana na kuwa na watu makini wenye uwezo wa kuingia serikalini na kuwatumikia Watanzania," anasema.

Katibu mkuu huyo anaongeza kuwa chama chao kina uzoefu wa kushirikiana na serikali katika uongozi, hivyo anaamini kuwa uteuzi wa mwanachama wao huyo, ni mwendelezo wa serikali kukiamini.

> "Labda nikukumbushe tu kwamba, chama chetu kimewahi kuwa sehemu ya serikali pale mwenyekiti wetu wa taifa Hamad Rashid Mohammed alipoteuliwa kuwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar," anakumbusha.

"Labda nikukumbushe tu kwamba, chama chetu kimewahi kuwa sehemu ya serikali pale mwenyekiti wetu wa taifa Hamad Rashid Mohammed alipoteuliwa kuwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar," anakumbusha.

Anaeleza kuwa Hamad aliendelea kuwa mwanachama wa ADC licha ya kuwa waziri serikalini, na kwamba anaamini kuwa hata kwa Queen itakuwa hivyo, kwa kuwa ukuu wa mkoa hauwezi kuingilia utendaji wake wa shughuli za chama.

"Kwa ujumla tumepokea kwa furaha uteuzi wake na sasa tunajiandaa kukaa vikao vya chama kwa ajili ya kutoa tamko la kumpongeza na kumtakia kazi njema," anasema kiongozi huyo.

Anafafanua kuwa, iwapo itatokea mkuu huyo wa mkoa akaamua kuhama chama kama ambavyo imewahi kutokea kwa baadhi ya wanachama wa upinzani walioingizwa serikalini, ADC haiwezi kumzuia.

### MAONI YAKE QUEEN

Akizungumza na gazeti hili baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo, Queen anasema, kwa sasa hawezi kuzungumza chochote, badala yake anasubiri hadi atakapoapishwa ndipo atoe ya moyoni.

"Kwanza bado sijaapishwa, hivyo ni vigumu kwangu kuzungumzia uteuzi huu wala hatima yangu kwenye chama changu cha ADC, ninaomba uvute subira hadi nitakapoapishwa ndipo nitakuwa na la kusema," anasema mteule huyo..

Aidha, mwanasiasa huyo amegusia kidogo uchaguzi mkuu wa mwaka jana kwamba, alijitosa akiamini kuwa kinamama wengi wanapopata nafasi ya kuingia katika nafasi mbalimbali za uongozi na ngazi za kutoa maamuzi, wanakuwa ni chachu na wahamasishaji.

"Maana yangu ni kwamba, wanakwenda kutengeneza usawa wa kijinsia kuhakikisha mwanamke na binti wa Tanzania anapata maendeleo na manufaa bila ya kujali jinsia yake," anasema.

Queen anasema, huo ndiyo ulikuwa msukumo wake uliomfanya ajitose, kwa kuwa nafasi ya mwanamke kwenye uongozi ni kubwa zaidi, kwa kuwa kina mama wengi wana sifa uongozi ambao ni wa kiuadilifu.

Anasema, wanawake wa sifa ya uongozi ambao hauna makandokando, na kwamba, tangu Tanzania ipate uhuru ilikuwa haijaongozwa na kiongozi mkubwa wa nchi wa jinsi ya kike na sasa amepatikana.

"Hayo ndiyo ninayoweza kukuambia kwa sasa, lakini suala la uteuzi wangu kuwa mkuu wa mkoa, ninaomba uniache kwanza, ili wakati mwafaka utakapofika, nitaongea kila kitu utakachoniuliza," anasema.

### MTAZAMO WA UTEUZI

Mchambuzi wa siasa, Abdulkarim Atiki, akizungumzia uteuzi huo, anasema mabadiliko na uteuzi wa wakuu wa mikoa uliofanywa na Rais Samia, unaendelea kuonyesha mwelekeo wa kisiasa kiuchumi na hasa kwenye suala la kushirikisha wengine kuleta maendeleo.

"Ikumbukwe kuwa amewahi kusema kuwa, anataka kila Mtanzania ashiriki kwenye shughuli za maendeleo ya nchi yake na kuimarisha demokrasia nchini, hivyo anatembea juu ya kile anachoamini," anasema Atiki.

Anafafanua kuwa Rais anatambua kwamba, nchi hii ni ya Watanzanai wote bila kujali itikadi za vyama, hivyo anaona kuna umuhimu wa kuwashirikisha kila mmoja kwa nafasi yake ili kuijenga nchi yao.

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa hatua ya Rais kuteua wapinzani kuingia serikalini ni moja ya hatua zake za kushirikisha Watanzania ili watoe mchango wao kwa ajili ya maendele yao na kusonga mbele.

"Niseme tu kwamba, kila zama na zina kitabu chake, hivyo ninaamini kuwa zama za Rais Samia nazo zina mambo yake, lakini lengo kuu ni kuhakikisha Tanzania inapiga hatua kwenda mbele zaidi," anasema.

# MILTON OBOTE
# RAIS ALIYEACHA HISTORIA YA KUPINDULIWA, AKAREJEA IKULU

**Na Christina Mwakangale**



Milton Obote, rais wa zamani wa Uganda, aliyepinduliwa akiwa ughaibuni na Iddi Amini Dadaa. **PICHA ZOTE MTANDAO.**



Iddi Amini 'aliyemtumbua' Obote akiwa nje ya nchi.

KWENYE historia ya miaka ya 1960 hadi 1980 imo kumbukumbu ya Apollo Milton Obote, ambaye ni rais pekee wa Uganda aliyeongoza nchi hiyo kwa vipindi viwili japo katika mihula tofauti awali akiwa amechaguliwa na wananchi na baadaye akiwa amerejea madarakani baada ya kupinduliwa.

Historia ya miaka 50 nyuma, inamkumbuka Obote kwa kukiuka katiba kuamua na kujitangaza kuwa rais. Ingawa Waganda watamkumbuka kuwa kiongozi aliyewaongoza kuipatia nchi yao uhuru, Oktoba 9, mwaka 1962 wana mengi yanayohusu kukengeuka kidemokrasia.

Obote, alikaa ikulu kwa vipindi tofauti yaani miaka 1960 na 1980. Alikuwa rais mwaka 1966 hadi 1971, lakini hapo awali alikuwa Waziri Mkuu wa Uganda kabla ya kushika nafasi ya urais kabla ya kupinduliwa na kuondolewa madarakani, kwake Obote haikuwa sababu ya kujaribu kukikalia tena kiti hicho.

Januari 25, mwaka 1971, akihudhiria mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola nchini Singapore, alipinduliwa na Idi Amin Dada. Ingawa Obote Aprili mwaka 1979, alimng'oa Idi Amin, baada ya vita ya Kagera.

Pia alikuwa rais kwa mara ya pili, kuanzia mwaka 1980 hadi 1985 kupinduliwa tena na wakuu wa jeshi lililokuwa likiongozwa na Jenerali Tito Okello na kwenda kuishi uhamishoni. Uchaguzi wa urais wa mwaka 1980 uliompa uongozi, licha ya kuwa na vikwazo, pamoja na kutokukubaliwa na vyama vya upinzani, akiwamo Yoweri Museveni kuanza harakati za kukiinua chama chake cha National Resistance Army (NRA) kupitia vita ya msituni dhidi ya Obote.

Katika vita hiyo serikali na jeshi la Obote, lilishtakiwa kwa makosa ya jinai dhidi ya haki za kibinadamu zilizosababisha vifo vya maelfu ya Waganda. Obote, alipata uungwaji mkono kupitia muungano wake wa chama alichokianzisha kilichoitwa Uganda People's Congress (UPC), na wanachama kutoka nchini kote na alifanikiwa kupata viti vingi bungeni.

Rais huyo alirudi madarakani mwaka 1980, kabla ya kupinduliwa na Yoweri Museveni baada ya miaka sita.

Licha ya kwamba Museveni alikuwa ni tawi la vijana la chama cha Obote cha UPC, alitumia njia mbalimbali ili kumshinda, Obote na kumwondoa madarakani. Kutokana na misukosuko ya kisiasa Obote amewahi kuishi uhamishoni katika nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania na Zambia.

Wanasiasa wa upinzani kama vile Kizza Besigye, ambaye kwa sasa ameachana na siasa aliwahi kusema kwamba, Uganda hakujawahi kuwapo ubadilishanaji madaraka kwa amani tangu uhuru wa nchi hiyo uliopatikana mwaka 1962.

### HISTORIA YA OBOTE

Milton Obote, alizaliwa Desemba 28, 1924, katika Kijiji cha Akoroko, Lango Kaskazini mwa Uganda. Akiwa ni mtoto wa tatu katika familia ya watoto 11 wa Stanley Opeto, chifu wa kijiji na mama yake aliitwa Puliska Opeto, walioishi eneo la kaskazini kati ya Uganda.

Alisoma Shule ya Msingi Ibuje iliyopo Lira na baadaye kuhamia Jinja na kisha kujiunga na Chuo cha Busoga kilichoko Mwiri na hatimaye Chuo Kikuu cha Makerere, jijini Kampala, kuanzia mwaka 1948 hadi 1949 akisomea uchumi kwa mwaka mmoja baada ya kufukuzwa

kabla ya kuhitimu, kutokana na harakati zake za kisiasa.

Hakuishia hapo alipata ufadhili wa masomo kutoka Uingereza na kwenda kusoma nchini Marekani na Ujerumani, na kisha kurudi Afrika mwaka 1950 na kuishi Kenya. Akiwa nchi jirani ya Kenya alikuwa mtumishi wa umma aliyejiunga na harakati za kutafuta uhuru wa nchi hiyo na kujiunga na Chama cha Kenya African Union (KANU).

Ilipofika Julai 1985, Obote alipinduliwa tena na jeshi na kukimbilia nchini Zambia hadi alipofariki dunia Oktoba 20, mwaka 2005, akiwa na umri wa miaka 79.

### MARAIS WENGINE

Rais wa kwanza wa taifa hilo ni Edward Luwangula Walugembe Mutesa wa Pili aliyeongoza tangu Oktoba 9, 1963 hadi Machi 2, 1966, akifuatiwa na Obote, mwingine ni Idi Amin Dada (Field Marshall), aliyeongoza kuanzia Januari 25, 1971 hadi Aprili 12, 1979.

Yusuf Kironde Lule aliongoza kuanzia Aprili 13, 1979 hadi Juni 20, 1979 Godfrey Lukongwa Binaisa kuanzia Juni 20,1979, hadi Mei 1980. Licha ya kwamba Obote aliongoza kwa vipindi tofauti na kisha Jenerali Tito Okello Lutwa aliongoza kuanzia Julai, 1985, hadi Januari 1986. Tangu mwaka 1986 aliyepo madarakani ni Yoweri Museni.

### URITHI WA OBOTE KIJESHI

Mtaalamu wa historia Frank Schubert anasema mapinduzi ya Obote yalibainisha wazi kabisa kwamba jeshi ni taasisi muhimu katika utatuzi wa matatizo ya ndani ya kisiasa na kwamba viongozi wa kisiasa kama Obote wasingeona haya kulitumia jeshi, hata kwa kulibebesha jukumu kubwa la kujiimarisha.

Kupitia jeshi lake la waasi ambao kwa sehemu kubwa walikuwa wanatokea magharibi mwa Uganda, alifanikiwa kulishinda jeshi la serikali lililokuwa linadhibitiwa kwa sehemu kubwa na maofisa kutoka kaskazini hasa Walango na Waacholi.

**MITANDAO**





# 'Kundi la vijana linaathiriwa zaidi ajali barabarani'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KUNDI la vijana linaathiriwa kwa kiasi kikubwa na ajali za barabarani kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutozingatia sheria za usalama barabarani.

Sababu nyingine ni kuendesha kwa mwendokasi, kutumia vilevi kunakoshawishi kuvunja sheria za usalama barabarani.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu, Habari na Mawasiliano kutoka Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA) Tanzania, Rama Msangi, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu wiki ya kimataifa ya usalama barabarani ambayo imeanza Mei 17 hadi 23, mwaka huu.

Alisema kundi hilo linaathiriwa na ajali kutokana na kujishughulisha na uzalishaji mali ikiwamo wanafunzi wanaokwenda shuleni.

"Kufanyika kwa wiki hii inatukumbusha jamii kuendelea kupata uelewa wa matumizi ya barabara na kutambua athari za ajali za barabarani, inalenga kufikisha elimu kwa wananchi ili barabara zetu ziwe salama, kwa kuwa usalama wa barabarani ni jukumu la kila mtu," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna jitihada zimefanywa na serikali na mashirika mbalimbali ili kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua.

"Jitihada zimekuwa zikizaa matunda, mwaka jana ajali zimeonekana kupungua na inaonesha jitihada hizo haziendi bure, tunaamini tunaweza kufanya vizuri zaidi ya tulivyofikia," alisema.

Msangi alisema jitihada hizo zinaamsha jamii kutambua jukumu la kukabiliana na ajali za barabarani ni la kila mtu na ana wajibu kushiriki.

Alishauri serikali kufanyia kazi maoni ya wadau ya kurekebisha sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 kutokana na kuwa na upungufu na kuhitaji maboresho yatakayodhibiti ajali hizo.

Katika ripoti ya usalama barabarani ya mwaka 2018, iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiria kuwa watu milioni 1.35 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na ajali za barabarani.

Ripoti inaeleza watoto wenye umri kati ya miaka 5-14 na vijana wenye umri ya miaka 15-29 ndio majeruhi wakubwa wa ajali za barabarani na kusababisha vifo vyao.

# Muswada kulinda taarifa binafsi na faragha mbioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, inakusudia kupeleka bungeni muswada utakaowezesha kutungwa sheria itakayolinda taarifa binafsi na faragha za wananchi.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizojitokeza katika semina ya wabunge kuhusu huduma za mawasiliano na intaneti iliyofanyika ukumbi wa Msekwa bungeni.

Alisema wizara haisikilizi maongezi ya mtu, lakini panapokuwapo matumizi mabaya ndio wanafanya hivyo.

"Mimi kama waziri siwezi kuingia kupekua nani aliwasiliana na nani, ila kwa sasa tupo kwenye mchakato wa kutunga sheria ili kulinda data au mawasiliano ya watumiaji wa mitandao ambapo tutaweka mifumo jinsi ya kulinda taarifa za wananchi kwa usalama na mawasiliano yao yawe faragha," alisema.

Aliwataka wabunge kuwa tayari pendekezo la muswada huo litakapowasilishwa bungeni kwa maslahi mapana ya taifa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabir Bakari, alisema Tanzania inajipanga kutumia huduma ya 5G na majaribio yatafanyika ili kuhakikisha kasi ya teknolojia inayotakiwa inapatikana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, aliitaka wizara kuliangalia Shirika la Simu Tanzania (TTCL) ili mawasiliano yawepo ya kutosha nchini.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson alisema TCRA ihakikishe wanawafikia wananchi wote kwa kuwa huduma ya mawasiliano ni jambo la msingi kwa jamii.




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (kushoto), akizungumza wakati Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ikiwasilisha taarifa kuhusu huduma za mawasiliano na intaneti kwa wabunge, Bungeni jijini Dodoma juzi. Kulia ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Seleman Kakoso. PICHA: PRISCA ULOMI

# Wapendekeza magonjwa yasiyo ya kuambukiza kupewa kipaumbele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na kuwapo kwa kasi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, wabunge wameshauri Bunge kuangalia namna ya kuweka kipaumbele kwenye magonjwa hayo ili serikali ipate msukumo wa kutenga fedha za kukabiliana nayo.

Ushauri huo waliutoa jana katika semina kwa wabunge wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI iliyoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa yasiyoambukiza (TANCDA), kuhusu magonjwa yanayosababisha vifo kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU).

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Bulaya, alisema asilimia kubwa ya vifo kwa sasa vinatokana na magonjwa hayo kutokana na taarifa wanazotoa wataalamu.

"Hii kamati yetu ilianzishwa kutokana na tatizo la ugonjwa wa HIV nchini, wajibu wetu kama wabunge tunaweza kupendekeza kwenye bunge kama tunavyopitisha bajeti ya UKIMWI na dawa za kulevya, tunaweza kuiita kamati yetu ya UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ili nao waanze kutengewa fedha," alisema.

Alisema ni wajibu wa Bunge kuona umuhimu huo kutokana na hali ilivyo na kupendekeza jina la kamati ibadilishwe jina kama ilivyo kwingine.

Naye Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya, alisema kuna umuhimu wa kamati hiyo kuweka msukumo kwa serikali ili itenge fedha kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa hayo.

"Huu ndio uwe mwelekeo wa kamati kwasababu huwezi kutenganisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza na HIV, kuwe na muunganiko utakaosaidia kuweka msukumo wa kutenga fedha," alisema.

Alisema masuala ya magonjwa hayo yamesahaulika na kumshauri mwenyekiti wa kamati hiyo kupeleka mapendekezo bungeni ili kamati hiyo ipewe majukumu ya kusimamia na kuishauri serikali kuhusu kukabiliana na magonjwa hayo. Awali, akitoa mada, daktari bingwa wa magonjwa hayo kutoka Hospitali ya Hindu Mandal, Prof. Kaushik Raimaiya, alisema magonjwa yasiyo ya kuambukiza ndio yanayochangia vifo kwa watu wanaoishi na VVU.

"Kwa watu wanaoishi na VVU matatizo ya moyo yanakuwa mara tatu zaidi ya wasio na VVU na zaidi ya asilimia 10 ya wagonjwa wenye UKIMWI wanapata kisukari, maana anapotumia dawa watu wanataka ale vizuri anenepe, lakini unamwongezea matatizo kwenye magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema.

Kadhalika, Daktari Bingwa wa ugonjwa wa kisukari, Prof. Andrew Swai, alisema wimbi la magonjwa yasiyo ya kuambukiza sio kwa wazee pekee sasa yapo kwa vijana.

"Katika kukabiliana nayo nchi zingine zimejaribu, lakini bado ni tatizo kwa sababu ya kutobadili mtindo wa maisha, jinsi tunavyoishi na vyakula tunavyokula ndio vinasababisha matatizo ya afya kwa asilimia 50," alisema.

Hata hivyo, alisema fedha nyingi zinakwenda kwenye magonjwa ya kuambukiza na si yasiyo ambukiza.

"Wazee wakienda kwenye hospitali au vituo vya kutolea huduma za afya hakuna dawa za sukari, shinikizo la damu la juu, lakini za malaria, ARVs zipo," alisema.

Alisema katika utafiti uliofanywa mwaka 2012, robo ya Watanzania shinikizo la damu ya juu inayozidi.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo, Dk. Tatizo Waane, kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, alisema magonjwa yasiyoambukiza yanashamiri na njia za kujikinga zinahitaji rasilimali nyingi, kuzuia na kutibu, lakini bado ni tatizo.

"Badala kuwa na mtindo bora wa maisha tunapenda matibabu hatupendi kubadili mfumo wetu wa maisha, tunafikiria wabunge mtusaidie kwa kuwa mna nafasi kubwa ya kusaidia kukabiliana nayo," alisema.



# Maelfu watoto wakosa chanjo ya mlango saratani ya kizazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wasichana 7,700 wenye umri wa miaka 14 katika Mkoa wa Mbeya, hawajapata chanjo ya kwanza ya kuwakinga na ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Huduma za Chanjo wa Mkoa wa Mbeya, Danford Barnaba, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wa mkoa huo kuhusu chanjo mbalimbali zinazotolewa na serikali.

Alisema sababu nyingine ya wasichana hao kutopata chanjo ni kukosekana kwa mawasiliano mazuri kati ya vituo vya afya na shule katika baadhi ya maeneo na kutofanyika kwa usajili wa wanafunzi kwa ajili ya chanjo kwenye baadhi ya shule.

Barnaba alisema sababu nyingine ni kuchelewesha usajili wa walengwa, hivyo kushindwa kuwapata wakati wa chanjo kutokana na wengi wao kuwa tayari wanakuwa wamemaliza masomo na kutawanyika katika maeneo tofauti.

Alisema katika mkoa huo walipanga kuwachanja wasichana 24,026, lakini waliopatikana wakati wa chanjo ya kwanza walikuwa 16,263 na ambao hawakupata chanjo hiyo walikuwa 7,763.

Alisema ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi ndiyo aina ya saratani ambayo inaongoza kwa kusababisha vifo nchini, huku saratani ya matiti ikiwa ndiyo inayoongoza kusababisha vifo duniani.

Alisema kuwa inakadiriwa kuwa wanawake 466,000 wamethibitika kuwa na tatizo la saratani hiyo ya mlango wa kizazi duniani huku kwa Tanzania pekee ikikadiriwa kuwa ni wanawake 670 ambao wamepata saratani hiyo.

Pamoja na kwamba wakati wa uchanjaji wa chanjo ya kwanza idadi hiyo ya wasichana hawakupata chanjo, pia tatizo kubwa huwa linatokea wakati wa kuchanja chanjo ya pili ambayo wengi zaidi huwa hawapatikani.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo la baadhi ya wasichana kutochanjwa, wamependekeza wasichana wote wanaofikisha umri wa miaka 14 wapatiwe chanjo ya kwanza na ya pili bila kujali tarehe zao za kuzaliwa.

Vilevile, alisema wanapendekeza halmashauri ziimarishe mawasiliano kati ya vituo vya kutolea huduma za afya, shule na jamii ili kuwezesha kuwafikia watoto wote kwa ajili ya chanjo zote.

Baadhi ya wanahabari waliohudhuria mafunzo hayo waliishauri serikali kuimarisha utoaji wa elimu kwa jamii ili kuwe na uelewa wa kutosha kuhusu chanjo hiyo ya kuwakinga wasichana na ugonjwa huo hatari.

Gabriel Mbwile alisema kuna uwezekano elimu ikawa inawafikia zaidi wananchi wanaoishi maeneo ya mjini kuliko vijijini.

Alishauri wataalamu hao kutumia mbinu mbadala za kufikisha elimu kwa jamii za vijijini ikiwamo kutembelea shule mbalimbali na kutoa elimu pamoja na kutumia mikutano ya vijiji.



Baadhi ya wafanyabiashara wa ndizi katika Soko la Tandali, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, wakifanya shughuli zao juzi kwenye mazingira yasiyosalama ya kunyeshewa na mvua na matope kutokana na soko hilo, kukosa miundombinu mizuri. PICHA: NEBART MSOKWA

# Warajisi wasiowajibika waonywa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA ya Kilimo, imewaonya warajisi wazembe wanaoshindwa kusimamia na kuwajibisha viongozi na Vyama vya Ushirika vya Wakulima (AMCOS) kutokana na kuwapo kwa ubadhirifu na usimamizi mbovu wa fedha na mali umma.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Beatus Malema, aliyasema hayo mkoani Mbeya wakati wa kikao cha wadau wa zao la kahawa wakiwamo wakulima na vyama vya ushirika, wajasiriamali, sekta binafsi kutoka mikoa ya Ruvuma, Songwe na Mbeya pamoja na bodi ya zao hilo.

Kikao hicho ambacho kiliandaliwa na Taasisi ya Cafe Afrika, kilikuwa na lengo la kuwakutanisha wadau wa kahawa ili kuboresha mnyororo wa thamani wa zao hilo ambao utawasaidia wakulima na wafanyabiashara kukabiliana na vikwazo, ikiwamo soko la uhakika na usimamizi mzuri wa vyama vya ushirika.

Malema alisema baadhi ya warajisi wamekuwa sehemu ya tatizo kwani wameshindwa kusimamia ipasavyo majukumu yao na ikiwamo kushughulikia migogoro kwa wakulima waliojiunga kwenye AMCOS, hali inayosababisha wakulima kufikisha malalamiko yao kwenye Wizara ya Kilimo.

"Serikali imeajiri warajisi kwa ajili ya kufuatilia na kutatua kero za wakulima walio kwenye Amcos na si kukaa maofisini, lakini sio kama ilivyo sasa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wakulima ambao hufika wizarani kuhitaji msaada wakati nyie mko kwenye maeneo hayo mmekuwa sehemu ya migogoro na ubadhirifu naomba mbadilike mara moja," alisema Malema.

Malema aliziagiza Bodi za Kahawa kujitathmini na kuweka mikakati kuhakikisha wanaongeza tija kuboresha uzalishaji wa miche bora ya zao la kahawa baada ya kuporomoka kwa ubora wa zao hilo na kuathiri soko la ndani na nje ya nchi.

Mikakati ya serikali sasa ni kutoa kipaumbele kwa zao la kahawa ili kuongeza tija ya uwapo wa masoko ya dunia na sambamba na kutoa teknolojia za kisasa ili uzalishaji wa kahawa ukidhi mahitaji ya soko la dunia na kumnufaisha mkulima.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Cafe Afrika, Dafosa Sanga, alisema lengo la mkutano huu ni kuwezesha bodi zinazosimamia wakulima wa kahawa kuboresha thamani ya zao hilo katika mnyororo wa thamani na kuboresha kiwango cha uzalishaji ili kuwasaidia wakulima waliojiunga kwenye vyama vya ushirika.

Alisema kwa mwaka 2020/2021 jumla ya wakulima 6,000 wamenufaika na elimu ya uzalishaji bora wa kahawa na kwamba lengo ni kuwafikia wakulima 24,000 wa kahawa nchini hususani kuwapatia elimu ya kilimo bora, upatikanaji wa pembejeo za kilimo sambamba na kukarabati mitambo 20 kwenye AMCOS.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kahawa (TCB), Kajivu Kisenge, alisema Tanzania inakabiliwa na kikwazo cha kuporomoka kwa uzalishaji wa zao hilo na kwamba kupitia kikao hicho bodi za kahawa hazinabudi kukaa meza moja na kuweka mikakati ya namna kilimo hicho kitakuwa na thamani na kuwanufaisha wakulima.

Miongoni mwa wakulima wa kahawa kutoka wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe, alisema kwa kiasi kikubwa wanategemea mvua, hivyo anapendekeza kuandaa sera ya maji kwenye maeneo ya milima kutengeneza mifumo ya ufikishaji wa rasilimali hiyo kutoka katika mito ambayo itawawezesha kuzalisha kwa tija kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

# Wananchi wafunguka migomo ya daladala

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya mgomo wa daladala uliodumu kwa muda wa wiki moja jijini Mbeya, wananchi wameiomba serikali kusuluhisha migogoro ya wasafirishaji mapema kabla haijaathiri shughuli za kiuchumi.

Madereva wa daladala waligoma wakiishinikiza serikali kutekeleza masharti 10 waliyoyatoa Machi mwaka huu likiwamo la kuziondoa pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) kwenye barabara kuu.

Mgomo huo ulimalizika juzi, baada ya serikali kukubali kutekeleza masharti hayo ambapo wamiliki wa daladala, wamiliki wa bajaji na viongozi wa serikali walifanya kikao cha siku nzima ambacho kilisaidia kumaliza mgogoro huo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi wa Jiji la Mbeya, walisema mgomo huo uliwatesa kutokana na kuwaongezea gharama za maisha. Mesia Mwaijande, mjasiriamali katika Soko la Sokomatola jijini Mbeya, alisema awali walikuwa wanatumia Sh. 1000 kusafirisha bidhaa zao kutoka Mbalizi mpaka Sokomatola, lakini baada ya mgomo kuanza gharama hizo zilipanda mpaka Sh. 4000.

Naye Baraka Njeje, alisema usajili wa bajaji unaharibu taswira ya Jiji la Mbeya kwa maelezo kuwa serikali imeyaondoa magari madogo ya kubeba abiria yanayobeba watu 16 aina ya Hiece na kutaka yasajiliwe mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria kuanzia 28 mpaka 30, lakini sasa hivi inasajili tena bajaji.

Alisema kitendo hicho kinaharibu utaratibu ndani ya jiji kwa maelezo kuwa asilimia kubwa ya madereva bajaji hawana elimu ya kutosha kuhusu usalama barabarani, hivyo huwa wanasababisha ajali.



## Serikali yatakiwa kuweka tahadhari uwanja wa ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Shaurimoyo, Hamza Hassan Juma, ameitaka serikali kuchukua tahadhari katika matumizi ya uwanja mpya wa ndege wa Kigunda uliopo Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuimarisha ulinzi ili kuepuka uchochoro kutumika kuingiza dawa za kulevya.

Alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia makadirio ya Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa Idara Maalumu za SMZ) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo miongoni mwa majukumu yake ni ulinzi wa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliipongeza serikali ya Zanzibar kwa uamuzi wake mzuri wa kuona upo umuhimu wa kujenga uwanja wa ndege utakaotumika katika matukio mbalimbali ikiwamo ya dharura kwa abiria pamoja na watalii.

Aidha, alisema uwanja huo utatumika kwa matumizi ya kurahisisha usafiri wa wageni ikiwemo watalii kwenda katika eneo hilo lenye hoteli nyingi za kitalii kwa kutumia ndege ndogo.

Aliitaka serikali kuchukua hatua za kuimarisha ulinzi katika Uwanja wa Ndege wa Kigunda ili kudhibiti matukio ya ulinzi na kuepuka uwanja huo kutumiwa kuingiza dawa za kulevya kwa wageni.

''Mheshimiwa Spika, tunaipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuitikia kilio chetu cha kuitaka kujenga uwanja mwingine ambao utasaidia kurahisisha huduma za watalii, lakini pia tunatahadharisha ulinzi kamili katika uwanja huu kwa ajili ya kudhibiti matukio ya uingizaji wa dawa za kulevya,'' alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda Asha Abdallah Mussa, alisema kuwapo kwa uwanja wa ndege wa Kigunda kwa kiasi kikubwa utarahisisha na kuimarisha huduma za watalii kuingia nchini na kufanya matembezi yao katika Ukanda wa Kaskazini ya Unguja.

Hata hivyo, alizitaka taasisi za ulinzi kuhakikisha uwanja huo mdogo unapatiwa huduma zote kamili za ulinzi, ikiwamo kuingia kwa watalii na kuondoka kwa ajili ya kudhibiti matukio ya uingizaji wa dawa za kulevya.

''Kuwapo kwa uwanja wa ndege wa Kigunda kwa kiasi kikubwa utarahisisha safari za watalii kuingia nchini pamoja na kuingiza mapato ya serikali,'' alisema.

# Uamuzi wa SMZ ugatuzi wawakuna Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuamua kuondoa mpango wa ugatuzi, baada ya kubainika mapungufu mengi ikiwamo kutetereka kwa taasisi zilizogatuliwa.

Akichangia makadirio, mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Idara, Maalumu za SMZ) kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, Abdalla Abasi Wadi, alisema uamuzi huo umeshusha mzigo uliokuwa umebebwa na tawala za mikoa na serikali za mitaa kusimamia uendeshaji wa taasisi hizo.

Alisema katika Jimbo la Nungwi kwa zaidi ya miaka miwili sasa zipo shule za msingi ambazo zimeshindwa kuezekwa na kufanyiwa ukarabati kutokana na halmashauri zilizokabidhiwa ugatuzi kukosa fedha za kutekeleza mradi huo.

Alisema ugatuzi ulikuwa mzigo mkubwa kwa halmashauri za serikali za mitaa, kwa sababu katika muundo wake hazina mapato ya fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza sekta ya elimu na afya ya msingi.

''Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi nachukua nafasi ya kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamuwa kufuta mpango wa ugatuzi ambao ulizipa mamlaka serikali za mitaa kusimamia ugatuzi wa kuendesha sekta ya afya, kilimo na elimu ya msingi na maandalizi,'' alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliitaka serikali kutoa sababu za kufuta mpango wa ugatuzi ili kujipanga vizuri.

Alisema mpango huo umelenga kufikisha huduma muhimu za kijamii kwa wananchi kama ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara, ambapo mafanikio makubwa yamepatikana kupitia halmashauri za serikali za mitaa.

''Mheshimiwa Spika, sina shaka na kufutwa kwa mpango wa ugatuzi, lakini serikali ni vizuri zaidi ikatoa sababu za kuondoshwa kwa mpango wa ugatuzi ili wananchi waweze kufahamu kilichotokea,'' alisema. Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa kitaifa, Mtumwa Peya Yussuf, aliupongeza uamuzi wa serikali kuondoa ugatuzi katika halmashauri kwa sababu ilikuwa ni mzigo mkubwa katika utekelezaji wake kufikia mafanikio.

''Mheshimiwa Spika, malalamiko yalikuwa mengi kutoka kwa watendaji wa taasisi zilizogatuliwa yaliyokuwa yakiwasilishwa kwetu kutoka kwa walimu na wafanyakazi wa sekta ya afya... mimi nimefurahi kuona serikali sasa imebeba majukumu yote yenyewe,'' alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Idara Maalumu ya SMZ), Masoud Ali Mohamed, alitangaza rasmi serikali kufuta mpango wa ugatuzi wa kufikisha huduma muhimu za kijamii na maendeleo kwenda kwa wananchi moja kwa moja kwa mwaka wa fedha 2021-2022, baada ya kubainika kwamba halmashauri za wilaya kushindwa kumudu utekelezaji wake wa kusimamia taasisi zilizogatuliwa.



Waziri wa Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Gavu (katikati) na Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar juzi. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Watendaji lawamani 'kubania' vibali shughuli za utamaduni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Gavu, ameitaka Wizara ya Tawala za Mikoa kuacha tabia ya watendaji wake kuwakatalia wananchi kutoa vibali vya ngoma kwa baadhi ya makabila yaliopo Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza utamaduni wao.

Watendaji hao wamekuwa wakiwakatalia wananchi hao kutekeleza utamaduni wao, ikiwamo kuwacheza wanawake wari na kuwatoa wanaume katika jando.Gavu, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia makadirio ya bajeti ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo, alisema amepokea malalamiko ya wananchi wenye asili ya Tanzania Bara katika jimbo lake kukataliwa kupewa vibali vya kutekeleza utamaduni wao wa shughuli za kimila kwa mujibu wa makabila yao.

Alisema katika jimbo lake wapo wananchi wenye makabila tofauti, wengi wenye asili ya Tanzania Bara ambao kwa nyakati tofauti huchukua nafasi ya kutekeleza tamaduni zao kwa mujibu wa imani zao. Gavu alisema makabila hayo wamekuwa wakilalamika kwa nini wamekuwa wakizuiliwa na kukataliwa kupewa kibali cha kufanya shughuli za kiutamaduni za ngoma zinazowahusu ikiwa ni mila zao na kulinda urithi wa kijadi.

''Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu Wamakonde kumcheza mtoto mwari ni sehemu ya utamaduni wao kwa ajili ya kumweka katika mazingira mazuri ya kutimiza majukumu yake vizuri,'' alisema.

Gavu alisema ni muhimu kutumia hekima zaidi ili kuepuka kuonekana kwamba kuna ubaguzi wa kuwazuia baadhi ya watu kutekeleza mila zao za kijadi huku, baadhi wakifanya shughuli zao pamoja na ngoma zao za jadi.

Alisema hajawahi kusikia wananchi wa Jimbo la Bumbwini wakikataliwa kibali cha kupiga ngoma maarufu ya pongwa ambayo ni sehemu ya utamaduni wa wakazi wake.

# Kagame ataka haki kesi ya Rusesabagina

**Kigali,** RWANDA

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame amesema anataka kuona haki inatendeka katika kesi ya Paul Rusesabagina, anayeelezwa kuwa shujaa katika filamu ya mwaka 2004 ya Hollywood ya Hotel Rwanda, kuhusu mauaji ya kimbari ya Rwanda.

Katika mahojiano na chombo cha habari cha Kifaransa, France 24, rais alionya vitendo vya 'kibaguzi' dhidi ya mifumo ya kimahakama.

"Ninataka kushuhudia mwenyewe haki katika kesi hiyo. Kwa nini unafikiria haki ni ya Ulaya au Marekani au kwa mwingine yeyote lakini sio sisi?

"Ni kama vile jambo pekee kuhusu haki nchini Rwanda au Afrika, lazima lisimamiwe na Ulaya au Marekani au sehemu nyingine. Hapana, hapana kabisa," alisema Rais Kagame.

Rusesabagina anakabiliwa na mashtaka ya ugaidi yanayohusiana na mashambulizi mabaya nchini Rwanda, mwaka 2018 na 2019, yaliyofanywa na FNL, kundi lililo chini ya mwamvuli wa muungano wa MRCD wa vyama vya upinzani ambao yeye ni makamu wa rais.

**BBC**

# Wakenya imani rastafari wataka haki ya bangi kiroho

**Nairobi,** KENYA

KIKUNDI kimoja cha imani ya Rasta, kimeenda mahakamani wakitaka kuruhusiwa kutumia bangi kwa madhumuni ya kiroho.

Jumuiya ya Rastafari ya Kenya, inayojitambulisha kama kikundi cha kidini kidogo, ilisema washiriki wake wanaishi kwa hofu kwa sababu ya sheria ambazo ni kikwazo kwa shughuli zao za kiroho.

Ilisema wanachama wake mara nyingi walikuwa wakinyanyaswa, kutishwa, na kupekuliwa bila sababu katika nyumba zao za binafsi au sehemu zilizotengwa.

Kikundi kilisema matumizi ya bangi yanaruhusiwa na imani yao ya Rastafari kwa madhumuni ya kiroho, dawa, mapishi na sherehe.

Mawakili Shadrack Wambui na Alexander Mwendwa walidai kuwa bangi ni sakramenti inayounganisha waumini na muumba wao. Waliwalaumu viongozi kwa kutohakikisha kwamba haki zao za kidini zinaheshimiwa.

Mwaka 2019, Mahakama Kuu Kenya, iliamua kwamba harakati za Rastafarian zilikuwa kikundi cha kidini kama vingine vyovyote hivyo wanapaswa kuchukuliwa kwa usawa.

Uamuzi huo ulifuatia kesi ambayo mwanaume mmoja aliishtaki shule kwa kumfukuza binti yake, kwa sababu alikuwa amesokota nywele.

Mzazi huyo alisema binti yake alikuwa na mtindo huo wa nywele, kwa sababu familia ilijiunga na imani ya Rastafarian.

**BBC**

# Mkutano kuokoa uchumi Afrika kufanyika Ufaransa

**Paris,** UFARANSA

VIONGOZI 30 kutoka Afrika na Ulaya, wanakutana Jumanne katika mji mkuu wa Ufaransa, Paris, na mashirika makubwa ya kimataifa ya kiuchumi, kwa mpango wa kujaribu kuokoa uchumi wa Afrika inayotishiwa baada ya janga la Covid-19.

Afrika ni bara lililookolewa kwa suala la afya, likiwa na vifo 130,000 tu kutokana na Covid-19 kati ya vifo karibu milioni 3.4 duniani kote.

Ingawa inakabiliwa na mdororo wa kiuchumi, licha ya kuepuka vifo vingi vinavyosababishwa na janga hilo.

Mkutano wa Paris ambao utaanza saa 7 mchana kwa saa za Ufaransa na Afrika ya Kati, chini ya uongozi wa Emmanuel Macron, utagawanywa katika vikao viwili, moja kuhusu suala la ufadhili na kushughulikia deni la umma na kikao kingine kuhusu sekta binafsi barani Afrika.

Rais wa Ufaransa, Emmanuela Macron atahitimisha mkutano huo kwa mkutano wa pamoja na waandishi wa habari na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU).

Wazo la mkutano huo juu ya Ufadhili wa Uchumi wa Afrika, uliibuka katika msimu wa joto mwaka jana, wakati Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), lilipokadiri kwamba bara hilo liko hatarini kukumbwa na ukosefu mkubwa wa ufadhili wa dola bilioni 290, ifikapo mwaka 2023. Ukuaji wa bara la Afrika, ambao uchumi wake ulishuka kwa mara ya kwanza katika nusu karne mwaka jana kwa sababu ya janga hilo, unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 3.4 mwaka huu na asilimia nne, mwaka 2022. Pia, madeni ya umma yanaiweka hatarini Afrika, kama umasikini, mwaka huu, waafrika milioni 39 walikumbwa na umaskini uliokithiri, kulingana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**RFI**



Kijana wa Kipalestina, akiangalia namna chumba chake kilivyoathiriwa na mashambulizi ya angani ya Israel jijini Gaza, jana. Inakadiriwa zaidi ya watu 200 wamepoteza maisha kutokana na mgogoro unaoendelea kati ya Israel na Palestina. **PICHA: AP**

# Israel na Hamas waendelea kushambuliana

**Gaza,** PALESTINA

ISRAEL ilidai kwamba, iliipiga Gaza kwa mashambulizi ya anga Jumatatu na kufanikiwa kumuua kamanda mwandamizi wa wanamgambo wa Palestina, huku wanamgambo wa Palestina wakifanya mashambulizi ya roketi dhidi kwa Israeli wakati ghasia katika eneo hilo zilipoingia wiki ya pili.

Tangu mapigano yalipoanza Mei 10, mwaka huu, Wapalestina wasiopungua 200 wameuawa, wakiwamo watoto wasiopungua 59 na wanawake 35, kulingana na Wizara ya Afya ya Gaza.

Waisraeli wasiopungua 10 wameuawa katika mashambulizi ya roketi, pamoja na mtoto wa miaka sita.

Jeshi la Israeli, lilisema liliharibu mahandaki ya kilomita zipatazo 15 huko Gaza yaliyotumiwa na Hamas, pamoja na jengo la gorofa tano, ambalo lilikuwa na wizara ya Masuala ya Kidini inayoendeshwa na Hamas na kumuua kamanda wa Jihad wa Kiislam wa Kaskazini mwa Gaza, Hussam Abu Harbeed.

Ikijibu mashambulizi, kundi la Jihad lilifyatua roketi katika mji wa pwani wa Israel wa Ashdod na watu saba walijeruhiwa kwa mujibu wa maafisa.

**VOA**

# TER STEGEN KUIKOSA EURO 2020




**BARCELONA,** Hispania

MARC-Andre ter Stegen amethibitisha atakosa kuichezea Ujerumani kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti lake.

Matokeo ya Jumapili ya kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Celta Vigo pale Camp Nou yalimaanisha Barcelona hawawezi tena kuwa kwenye mbio za kuwania taji la LaLiga, huku Ter Stegen akiamua kumaliza msimu wake mapema kwa kufanyiwa upasuaji.

Taarifa fupi iliyotolewa na Ter Stegen ilisema atafanyiwa upasuaji wa goti la mguu wa kulia Alhamisi Mei 20, mwaka huu mjini Malmo na daktari Hakan Alfredson chini ya usimamizi wa madaktari wa klabu yake.

Wakati Barca haikutaja muda wa kurudi dimbani, Ter Stegen mwenyewe aliposti kwenye ukurasa wake wa Instagram Jumatatu akithibitisha kuwa hatakuwa kwenye michuano ya Euro 2020.

"Nimekatishwa tamaa kuhusu kipigo cha juzi (Jumapili) na kwamba hatutaweza tena kushinda taji la LaLiga," aliandika.

"Baada ya mwanzo mgumu wa msimu huu, tulionyesha mwamko mzuri tukicheza mechi 19 bila kufungwa - lakini hatukuwa na uwezo wa kuendelea kuwa kwenye kiwango kile.

"Nimeamua pamoja na timu ya madaktari kwamba, nitafanyiwa upasuaji wa goti langu la kulia na nitaikosa michuano ya Euro 2020."

# Barcelona yafikiria kumtimua Koeman

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA ipo kwenye harakati za kutafuta mrithi wa kocha, Ronald Koeman kwa mujibu wa ESPN.

Rais wa Barca, Joan Laporta anataka kumfukuza raia huyo wa Uholanzi, lakini hadi kwanza apate mrithi wa kukinoa kikosi hicho cha Katalunya.

Barca iliondolewa rasmi kwenye mbio za ubingwa wa LaLiga baada ya kipigo cha Jumapili na sasa mbio hizo zimebakia kwa Atletico Madrid na Real Madrid.

Hata hivyo, Koeman, ambaye aliisaidia Barca kushinda taji la Copa del Rey mapema mwezi uliopita amebakia mwaka mmoja kwenye mkataba wake. Chanzo kimoja kimeitonya ESPN kwamba, Koeman anatafutiwa mbadala wake mwishoni mwa msimu huu.

Ernesto Valverde alifukuzwa mwaka 2020 na nafasi yake ikachukuliwa na Quique Setien kabla ya Koeman kupewa mikoba hiyo.

Majina ya Xavi Hernandez, Mauricio Pochettino na Erik ten Hag yanatajwa katika kibarua hicho.





## *Nyumba ya Neymar yavamiwa*

**PARIS,** Ufaransa

MTU MMOJA akiwa na biblia alivamia na kuingia katika nyumba ya Neymar mapema Jumapili kabla ya kukamatwa na kupelekwa hospitali ya matatizo ya saikolojia, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mtu huyo mwenye umri wa miaka 26 aliingia kwenye bustani ya Neymar katika nyumba yake iliyopo La Celle-Saint-Cloud Magharibi mwa jiji la Paris na kuruka ukuta kuingia ndani.

Alibakia mita chache kufikia mlango mkubwa kabla ya walinzi kumwona na kuwahi kumkamata na kupelekwa kituo cha polisi cha Bougival.

Aliwaambia polisi kwamba alitaka kumpa Neymar "neno la Mungu."

Kwa mujibu wa ripoti alisema kuwa hakuwa na nia ya kuiba chochote, kwani alitaka tu kuzungumza mambo ya dini na Neymar.

Nyota huyo namba 10 wa Brazil ni mchezaji mwingine wa PSG ambaye nyumba yake ilivamiwa na watu, ingawa lilikuwa tukio tofauti.

Machi mwaka huu, ghorofa la Angel Di Maria lilivamiwa wakati mke na watoto wake wawili wakiwa ndani na yeye akiwa dimbani pale Parc des Princes kucheza dhidi ya Nantes.

Baba na dada wa mlinzi, Marquinhos pia walivamiwa nyumbani kwao jijini Paris.

## HABARI MICHEZO

# Mancini aongeza mkataba Italia

**ROME,** Italia

ROBERTO Mancini amepewa mkataba mpya na Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), na sasa atakinoa kikosi chanchi hiyo hadi baada ya fainali za Kombe la Dunia mwaka 2026.

Mancini aliteuliwa kuwa kocha wa Italia Mei mwaka 2018, akichukua nafasi ya Luigi Di Biagio ambaye alichukua mikoba hiyo kutoka kwa Gian Piero Ventura.

Ventura alishindwa kuiongoza Italia kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2018, baada ya Azzurri hao kufungwa kwenye kapu la kufuzu na Sweden.

Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza Italia kushindwa kufuzu Kombe la Dunia tangu mwaka 1958 na FIGC ikaamua kumteua Mancini kuchukua mikoba hiyo.

Awali aliteuliwa kuinoa timu hiyo hadi mwaka 2020, lakini akaongezwa baada ya michuano ya Euro 2020 kuahirishwa.

Akapewa mkataba hadi baada ya Kombe la Dunia mwaka 2022, lakini sasa FIGC wameamua kumwongezea Mancini miaka minne zaidi.

Rais wa FIGC, Gabriele Gravina alinukuliwa akisema: "Ni mafanikio makubwa na ni uwekezaji wa muda mrefu kwa ajili ya timu ya taifa.

"Nina furaha kubwa, kwa sababu Roberto anaijua vizuri kazi iliyopo mbele yake kwa sasa."





# RONALDO: NATAKA NIKUMBUKWE VIZURI

**TURIN,** Italia

CRISTINO Ronaldo anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa muda wote duniani, na nyota huyo wa Ureno ana furaha kuwa sehemu ya historia ya mchezo huo.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36 na mshindi mara tano wa Ballon d'Or amebainisha kwamba anataka kukumbukwa wakati atakapokuwa ametundika daruga zake, wakati akizungumza mtandao wa livescore.com ambao umemteua kuwa balozi wake.

Alisema: "Natumaini nitakumbukwa siku moja kama mmoja wa wachezaji wakubwa duniani, mtu ambaye alijituma sana.

"Ambaye mara zote alifanya awezalo kusaidia timu yake na kuwa sehemu ya historia ya mchezo huu."

Pia akawatambua wachezaji ambao anaamini watafuata nyayo zake kwa miaka inayokuja. Ronaldo aliongeza: "Ni ngumu kuchagua mchezaji mmoja kusema huyu atakuwa bora sana baadaye.

"Lakini nafikiri navutia kupata kizazi kipya cha wachezaji kama (Erling) Haaland na (Kylian) Mbappe, ambao naona watakuwa bora sana baadaye."

# *Hatima ya Mata United haifahamiki*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer hana uhakika kama Juan Mata atabakia Old Trafford baada ya msimu huu.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania ametumia kipindi cha miaka saba na nusu hapo Old Trafford, akicheza mechi 271 kwa kipindi hicho.

Hata hivyo, amekuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza msimu huu - akicheza mechi 16 tu katika mashindano yote - na atakuwa huru mwezi ujao.

United ina kipengele cha kuongeza miezi 12 katika mkataba wa Mata, lakini Solskjaer amesisitiza mchezaji mwenyewe ndio mwenye uamuzi wa mwisho kuhusu majaliwa yake.


"Nimekuwa na mjadala na Juan na tutazungumza tena hivi karibuni," alisema Solskajaer katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Bila shaka, hajacheza mechi nyingi na angependa kucheza mara kwa mara, uamuzi wa kubaki au kuondoka utafanywa na yeye. "Yeye ndio mwenye uamuzi wa mwisho kuhusu majaliwa yake na amekuwa mtumishi mzuri wa klabu hii.

"Lakini ni ngumu kwake kukaa bila kucheza, kama nilivyosema kuwaacha wachezaji wazuri pia inakuwa ngumu kwa timu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KANE ATANGAZA KUONDOKA SPURS

## Uamuzi wake unatokana na kuhitaji changamoto mpya na kutimiza ndoto za kushinda...

**LONDON,** England

TOTTENHAM Hotspur imeshauri "kila mmoja" kujikita kwenye kumalizia vizuri Ligi Kuu England kwa msimu wa 2020-21, huku ripoti ikibainisha kwamba, Harry Kane ameitaarifu klabu hiyo anataka kuondoka.

Kane ambaye ni zao la akademi ya Spurs amejiimarisha kama mmoja wa mastraika bora duniani, lakini kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita klabu hiyo imekuwa kwenye wakati mgumu kutimiza malengo yake.

Nahodha huyo wa England amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Tottenham kwa miaka kadhaa.

**Sky Sports ilidai Jumatatu kwamba, Kane ameiambia klabu hiyo anataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu, kwa ajili ya kwenda kusaka mataji.**

Spurs haijashinda taji lolote tangu lile la EFL msimu wa 2007-08, huku Kane akiwa sehemu ya kikosi kilichofungwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19 na fainali ya EFL msimu huu.

Amebainisha kwamba anahitaji changamoto mpya baada ya kufungwa na Manchester City kwenye fainali ya EFL mwezi uliopita wakati alipotangazwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu England.

Alisema: "Taji binafsi ni zuri, ni mafanikio ya kuvutia. Labda wakati nikiangalia nyuma kwenye kipindi changu cha uchezaji naweza kusema kuna kitu bado sijakifanya.

"Lengo kubwa kwa mchezaji ni kushinda taji kubwa na timu, kwa kadri inavyowezekana, na sasa nataka kushinda zawadi kubwa."

## ZISIKUPITE

### MENDES AGOMBEWA EPL

MANCHESTER United itashindana na Manchester City katika kuwania saini ya mlinzi kinda wa Sporting Lisbon, Nuno Mendes kwa dau la pauni milioni 52. ***(Mail)***

### MORENO AINGIA SOKONI

LEEDS United na Rangers ya Scotland wanamfuatilia kwa karibu mchezaji wa klabu ya America de Cali mwenye umri wa miaka 21 raia wa Colombia, Santiago Moreno. ***(Football Insider)***

### TRIPPIER KUREJEA ENGLAND

NYOTA wa England, Kieran Trippier amehusishwa na hatua ya kurudi katika Ligi Kuu England, huku Manchester United na Everton zote zikishindana kupata saini ya beki huyo wa kulia kutoka Atletico Madrid. ***(Athletic, subscription required)***

### DAU LA BISSOUMA NJE

KLABU ya Brighton & Hove Albion imeziambia Liverpool na Arsenal itachukua dau la pauni milioni 40 ili kumwachia kiungo wa kati wa Mali, mwenye umri wa miaka 24, Yves Bissouma. ***(Sun)***

### SULEMANA ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inaiongoza Ajax katika mbio za kumsaini mshambuliaji wa Ghana, Kamaldeen Sulemana, 19, kutoka FC Nordsjaelland baada ya mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo siku ya Jumatatu. ***(Football Insider)***

### ALONSO, PALMIERI KUONDOKA

MLINZI wa Hispania, Marcos Alonso (30) na beki wa kushoto wa Italia, Emerson Palmieri, 26, wanapigania kuondoka Chelsea mwisho wa msimu huu ili kujaribu kutafuta fursa katika Ligi Kuu Italia, Serie A.***(Mail)***

### KANE AGOMBEWA

KLABU za Manchester City, Chelsea na Manchester United zimeonyesha hamu ya kutaka kumsajili fowadi wa Tottenham Hotsput, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

### AANHOLT NJIA MOJA

MLINZI wa Uholanzi, Patrick van Aanholt mwenye umri wa miaka 30, anatarajiwa kuondoka Crystal Palace wakati mkataba wake utakapofikia mwisho. ***(Athletic, subscription required)***

### DEPAY KUTUA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay (27), anatarajiwa kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na klabu ya Barcelona kwa uhamisho huru ifikapo mwisho wa msimu huu. ***(L'Equipe)***

### GERVINHO KWENDA UTURUKI

NYOTA wa Ivory Coast na aliyekuwa mshambuliaji wa Arsenal, Gervinho mwenye umri wa miaka 33, anatarajiwa kuondoka katika klabu ya Parma ya Italia mwisho wa msimu huu ili kujiunga na Trabzonspor ya Uturuki. ***(Goal)***

## Waluguru, Bogoz, Sky jukwaa moja

**Na Sabato Kasika**

BENDI tatu za muziki wa dansi zinatarajia kufanya onyesho la pamoja ikiwa ni moja ya mikakati inayoandaliwa na wadau wa muziki huo yenye lengo la kuirejesha tasnia hiyo katika nafasi yake ya juu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Onyesho hilo linatarajiwa kufanyika Mei 29, mwaka huu, mkoani Morogoro na litashirikisha bendi za Waluguru Original, Bogos ya Dar es Salaam na Sky Melody ya jijini Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili, mmoja wa waandaaji wa onyesho hilo, ambaye ni Mkurugenzi wa Waluguru Original, Deogratius David 'Killer Man', alisema maandalizi ya onyesho hilo yanaendelea vizuri.

"Ukweli muziki wa dansi umeshuka sana, hivyo kuna haja ya wanamuziki kuwa na mikakati ya kuurudisha kwenye chati, ndiyo maana tunaandaa onyesho la pamoja ikiwa ni moja ya mikakati hiyo," alisema KillerMan.

Kiongozi huyo alisema wanaamini kufanyika kwa onyesho hilo kutakuwa ndio mwanzo wa kurudisha muziki huo kwenye 'chati' na kuwapa mashabiki wao burudani ya kiwango cha juu.

## Dulla Mbabe ulingoni Urusi

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Pazi maarufu Dulla Mbabe anatarajiwa kupanda ulingoni kuchuana na Silya Gin katika pambano litakalofanyika leo katika mji wa Moscow nchini Urusi.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Dulla Mbabe alisema amejipanga vizuri kumpiga mpinzani wake katika pambano hilo la kuwania mkanda unaotambulika na Shirikisho la Kimataifa ya Ngumi la WBC.

Bondia huyo alisema alimfuatilia mpinzani wake kwa muda mrefu kupitia mapambano mengine aliyoyacheza na kuongeza amejipanga kumdhibiti na hatimaye kumshinda akiwa nyumbani kwao.

Naye Kocha wa bondia huyo, Omari Dame aliliambia gazeti hili hana wasiwasi na bondia wake kutokana na mazoezi ya muda mrefu aliyofanya anaimani atarudi na mkanda wa pambano hilo.

"Sina wasiwasi na bondia wangu kutokana na mazoezi niliyompa, nina matumaini ataibuka na ushindi kwa sababu tumemsoma kwa kipindi kirefu na kufahamu ubora na mapungufu yake, tutarajie matokeo bora kutoka kwa bondia wangu," alisema kocha huyo.

# MASHABIKI WAIPOKEA GEITA GOLD FC KIFALME

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanikiwa kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, maelfu ya mashabiki wa soka mkoani Geita walijitokeza kwa wingi kuipokea timu yao ya Geita Gold FC iliyokuwa inatokea Gairo mkoani Morogoro katika mechi yake ya mwisho ya msimu.

**Geita Gold ilimaliza msimu kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Gairo.**

Mashabiki wa soka mkoani humo, wakiwa kwa miguu na pikipiki waliwalaki wachezaji wao waliokuwa kwenye basi, pamoja na viongozi kwa ngoma, chereko na hoi hoi walipokuwa wakiingia kwenye ardhi ya mkoa huo.

"Ligi ilikuwa ngumu, lakini tumefanikiwa kupanda, tunashukuru kwa hili," alisema Fred Felix Minziro, Kocha Mkuu wa kikosi hicho ambaye anaingia kwenye rekodi ya kuzipandisha timu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wananchi wa mkoa huo waliwashukuru wachezaji na viongozi, Halmashauri ya Mji wa Geita, Wilaya, pamoja na Mkuu wa Mkoa huyo, Dobert Dimian kwa ushirikiano mkubwa baina yao na kusababisha timu isiwe na matatizo yoyote katika msimu mzima.

Timu hiyo ilishindwa kupanda Ligi Kuu misimu miwili mfululizo iliyopita, ilipokuwa inakwamia kwenye mechi za mtoano maarufu 'play off'.

Alikuwa ni mchezaji wa zamani wa Mbao FC na Kagera Sugar, Venance Ludovic aliyepachika mabao yote mawili dakika ya 20 kwa mkwaju wa penalti na dakika ya 37 na kuifanya Geita Gold kumaliza kinara katika Kundi B na kukata tiketi ya kupanda daraja moja kwa moja.

Kwa ushindi huo, Geita Gold imepanda Ligi Kuu baada ya kujikusanyia pointi 37 na kuongoza Kundi B.

Kikosi hicho cha Minziro kimeungana na Mbeya Kwanza ambayo ilikuwa ya kwanza kupata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuongoza katika Kundi A.

Timu nyingine zitakazopanda daraja zitajulikana baada ya kumalizika kwa mechi mbili za mtoano zitakazowakutanisha klabu za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza kutoka katika Kundi A na B.



Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo (katikati), akimvisha medali nahodha wa timu ya watoto ya wasichana ya mchezo huo, Jonada Omuteku (kushoto), baada ya kumalizika kwa mchakato wa kugawa zawadi kwa wachezaji waliofanya vizuri katika shindano la watoto lililofanyika Jumapili iliyopita katika klabu hiyo jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# *Gwambina yaajiri kocha Mmarekani*

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Sofapaka na Wazito FC ya Kenya, Mmarekani Melis Medo, anatarajiwa kusaini mkataba wa kuifundisha Gwambina FC kwa ajili ya kuinusuru timu hiyo kuendelea kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili kutoka kwa Gwambina zinasema Medo aliwasili nchini juzi jioni kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo na mabosi wa klabu hiyo yenye makazi yake jijini Mwanza.

Chanzo hicho kilisema kocha huyo ameshaanza kazi baada ya kutambulishwa rasmi kwa wachezaji wa timu hiyo katika mazoezi yaliyofanyika jana asubuhi.

"Medo alikuwa miongoni mwa walimu ambao walituma wasifu wao muda mrefu, kwa kipindi hicho tulikuwa tunahitaji zaidi makocha wazawa, ila baada ya kuondoka kwa Mohammed Badru, ikabidi tuwasiliane naye na amekubaliana na mahitaji yetu.

"Makubaliano yetu ya awali ni kumalizia msimu huu na kuhakikisha anaibakiza timu katika ligi na baada ya hapo tutaingia mkataba wa muda mrefu, kwa ajili ya msimu ujao," alisema kigogo mmoja wa Gwambina ambaye hakutaka kuweka wazi jina lake.

Aliongeza tayari wameanza mchakato wa kumtafutia vibali vyote vya kumruhusu kufanya kazi hapa na kuishi hapa nchini kama taratibu zinavyoelekeza.

Katibu Mkuu wa Gwambina, Daniel Kilai aliliambia gazeti hili ni mapema kulizungumza suala hilo na kuongeza mambo yatakapokuwa sawa watamtambulisha rasmi mrithi huyo wa Mohamed Badru.

Medo ambaye ana leseni B ya UEFA amepewa dhamana ya kuinusuru Gwambina FC isishuke daraja baada ya timu hiyo kushika nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiwa na pointi 30.

Michezo

Jumatano Mei 19, 2021

Nipashe



Kane atangaza kuondoka Spurs UKURASA 22



Wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Yanga wakiwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walipotembelea jijini Dodoma jana. Kikosi cha Yanga kinatarajia kupambana na wenyeji JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri. **PICHA: MTANDAO**

## Simba: Hesabu zitakubali

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kikosi chake kinaendelea na mazoezi vyema na anaamini 'hesabu zitakubali' na timu yake itasonga mbele katika mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika licha ya kupata matokeo mabaya Jumamosi iliyopita ugenini Afrika Kusini.

Gomes ambaye ni raia wa Ufaransa alisema utulivu mkubwa unahitajika katika mechi hiyo ya marudiano na 'maajabu' yanaweza kutokea na kuwaondoa wapinzani wao.

"Zile zilikuwa dakika 90 za kwanza, sasa tunajiandaa na dakika 90 nyingine, njia ni nyeupe kwa kila mmoja, tunaweza kufanya zaidi ya walichofanya wenzetu, kikubwa tunarekodi nzuri tukicheza nyumbani, tunaweza," Gomes alisema.

Kocha huyo alisema sayansi ya mpira iko wazi, unapofanya makosa mpinzani wako anayatumia mapungufu hayo kukuadhibu, hivyo wamejipanga kutorudia makosa waliyofanya katika mechi iliyopita.

"Tulifungwa siyo kwa sababu hatukucheza vizuri, wenzetu walitumia vyema mwanya walioupata, kwa kifupi tulikuwa bora uwanjani na tulifanya kila kitu tulichopanga ila bahati haikuwa kwetu, hiyo ndiyo tafsiri ya soka, hakuna ambaye anaweza kulitabiri."

# Yanga yafuata baraka Bungeni

### Kwa ajili ya kuwakabili JKT Tanzania ili kurejesha matumaini katika...

**Saada Akida na Augusta Njoji,**
DODOMA

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea kwa JKT Tanzania kuwakaribisha Yanga katika mchezo wa raundi ya 30 utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapo, huku wageni hao wakitokea bungeni walikokwenda kwa mwaliko maalumu, imefahamika.

**Yanga itashuka katika mechi ya leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 walioupata katika mchezo wa kwanza, lakini ikilazimishwa suluhu na Namungo kwenye mechi yao iliyopita ya ligi hiyo inayoelekea ukingoni.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi hiyo na lengo lao ni kuondoka na pointi tatu muhimu hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea ya kumaliza msimu huu wakiwa mabingwa.

Nabi alisema makosa waliyofanya katika mechi iliyopita yamerekebishwa na kila mchezaji amejipanga kubadilisha 'upepo' wa kutoka ushindi walionao.

"Bado tuna kazi ya kufanya, kwa sasa akili za wachezaji na benchi la ufundi ni kwenye mechi zetu zote ikiwamo ya kesho (leo) dhidi ya JKT Tanzania, malengo yetu ni kufanya vizuri, bado tunadhamira ya kupambana hadi mwisho," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema ana imani mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila upande unahitaji kuvuna pointi tatu ili kujiimarisha katika malengo lakini wapinzani wao wakihitaji kulipa kisasi cha kufungwa ugenini.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah 'Baresi', alisema kikosi chake kipo imara na watashuka uwanjani kwa jukumu moja la kutafuta pointi tatu muhimu katika mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10: 00 jioni.

Baresi alisema anafahamu mechi hiyo ni muhimu kwa kila upande na wachezaji wake wamedhamiria kuzibakisha pointi Dodoma na kuongeza matumaini ya kujinasua na janga la kushuka daraja.

"Ni mechi ngumu na itakayokuwa na ushindani mkubwa, tumejiandaa vizuri kwa ajili ya kupambana ili kutafuta ushindi na kubakia na pointi muhimu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi, tumejipanga kutumia vyema uwanja wa nyumbani, " alisema Baresi.

Yanga ilitinga bungeni lakini ziara yao iligubikwa na vijembe walivyorushiana wabunge ambao ni mashabiki wa Simba na Yanga.

Moja ya vijembe hivyo, wabunge hao waliambiana 'Subirini tarehe', wakimaanisha siku mpya iliyopangwa ya mechi ya watani wa jadi itakayochezwa ifikapo Julai 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hali hiyo ilijitokeza bungeni baada ya timu hiyo na viongozi wake kutambulishwa na Naibu Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson.

Akitambulisha wageni hao waliotembelea bunge jana, Dk.Tulia alisema "Wageni 36 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni viongozi na wachezaji wa timu ya wananchi, Yanga wakiongozwa na kiongozi wa timu hiyo Injinia Hersi."

Naibu Spika huyo aliwatuliza wabunge kutokana na shangwe vilivyoambatana na vijembe na kuwaeleza wachezaji hao hali hiyo inaonyesha namna wabunge walivyo pamoja nao.

"Mnafanya vizuri, jana walikuja hapa wachezaji wa Simba Queens nadhani tukubaliane nyie (Simba) mmeshindwa makofi, Yanga wamewashinda sasa hilo tukubaliane, sasa tusikilizane."

"Sisi tunatamani timu zetu ziendelee kufanya vizuri hapa ndani ya nchi na nje ya nchi, na naamini ujio wao na makofi ya waheshimiwa wabunge yanaashiria timu yenu itakapoenda nje ambayo hiyo nafasi wameipata kupitia Simba mambo yatakwenda vizuri," alisema.

Dk. Tulia alisisitiza "Timu zetu zinafanya vizuri na sisi tunatamani Simba inavyoenda nje ifanye vizuri na Yanga itakapoenda nje pia ifanye vizuri kwa hiyo timu zote zifanye vizuri na taifa lisonge mbele, karibuni sana...wabunge tulieni tumeshakubaliana kwamba Yanga humu ndani wametisha."

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Gwambina FC dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Gwambina Complex, ulioko Misungwi nje kidogo ya jiji la Mwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >